Nipashe

Ijumaa Julai 26, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579980

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

Ushahidi wa video kesi ya kina Mbowe watinga kortini

UKURASA 3

UKURASA 13

Lissu akata tiketi kurejea Tanzania

• **Azungumzia** mpango wa kesi kupinga kuenguliwa ubunge, asema kumshtaki Spika Ndugai kunahitaji umakini...*Ukurasa 2*

YALIYOMO

UKURASA WA 8

MAJALIWA ATANGAZA FURSA UWEKEZAJI RUVUMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amehamasisha wawekezaji kuwekeza mkoani...

UKURASA WA 26

WAZIRI ASHTUSHWA UHABA WA MBWA UWANJA NDEGE

UPUNGUFU wa mbwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius...

Mashine kamari zanaswa ukwepaji wa kodi

UKURASA 3

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akimjulia hali mmoja kati ya watoto 20, waliofanyiwa upasuaji wa moyo kwa ufadhili wake, katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, jijini humo jana. **Habari zaidi uk 3. PICHA: GETRUDE MPEZYA**

NSSF kuanza kuwasaka waajiri wakaidi michango

UKURASA 2

Lissu akata tiketi kurejea Tanzania

Na Enock Charles

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amesema maandalizi ya kurejea kwake nchini yamekamilika.

Vilevile, mtaalamu huyo wa sheria ameendelea kusisitiza kuwa kufungua kesi Mahakama Kuu kumshtaki Spika wa Bunge, Job Ndugai, kunahitaji umakini mkubwa.

Akizungumza na Nipashe kwa simu juzi akiwa Ubelgiji, mtaalamu huyo wa sheria alisema atarejea nchini Septemba 7, mwaka huu, kama alivyoeleza awali.

Mwanasheria huyo alisema ameshafanya maandalizi yote muhimu ikiwamo kukata tiketi ya ndege itakayomrejesha nchini siku hiyo.

"Uhakika wa nini? Unataka nikuonyeshe tiketi ya ndege? Ninayo tayari na mpango wa kurejea upo palepale kama nilivyosema, ukisikia vinginevyo, niulize," alisisitiza.

Lissu anayetajwa kuwa huenda akapewa nafasi ya kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani, pia alisema yuko mbioni kukamilisha taratibu za kufungua kesi kortini kumshtaki Spika Ndugai kwa kumvua ubunge.

"Mpango wa kufungua kesi hiyo taratibu zinaendelea maana inahitaji umakini mkubwa," Lissu alisema.

Mchana wa Septemba 7, 2017, Lissu (51), alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana wakati akijiandaa kushuka kwenye gari lake, nyumbani kwake Area D jijini Dodoma, akitokea bungeni kushiriki kikao cha chombo hicho cha kutunga sheria.

Baada ya shambulio hilo la kinyama, Lissu ambaye pia ni Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Bungeni, alilazimika kupatiwa matibabu ya kibingwa yaliyoanzia Hospitali ya Rufani ya Dodoma na siku hiyo hiyo usiku alihamishiwa katika Hospitali ya Nairobi, Kenya.

Lissu alikaa siku 121 katika hospitali hiyo ya Kenya hadi Januari 6, mwaka jana, alipohamishiwa Ubelgiji ambako Desemba 31, alimaliza matibabu yake ya awali na kuanza ziara katika baadhi ya nchi za Ulaya na Amerika.

Januari 19, mwaka huu, Lissu alihojiwa katika kipindi cha Dira ya Dunia cha Idhaa ya Kiswahili ya BBC na kuonyesha nia ya kugombea urais mwakani kama wanachama na viongozi wenzake wa Chadema watampa ridhaa hiyo.

Januari 21, mwaka huu, Lissu alihojiwa kwenye kipindi cha HardTalk cha BBC na mtangazaji maarufu Stephen Sackur, kipindi ambacho kilizua mjadala mkubwa kutokana na namna alivyojibu maswali.

Februari 20, mwaka huu, Lissu alifanyiwa upasuaji wa 23 aliodai ni wa mwisho kwenye goti la mguu wa kulia katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Leuven, Gasthuisberg, Ubelgiji na akasisitiza kuwa baada ya upasuaji huo atarejea Tanzania.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni (kulia), akiongozana na maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama, alipofanya ziara ya kukagua sehemu mbalimbali za kupitishia mizigo, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WMN**

JPM asafiri kwa treni

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli jana alisafiri kwa treni ya Tazara kutoka jijini Dar es Salaam kwenda Kisaki mkoani Morogoro na baadaye atakwenda Rufiji mkoani Pwani kuweka jiwe la msingi katika mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge.

Kabla ya kupanda treni, Rais Magufuli ambaye aliongozana na mkewe, Mama Janeth Magufuli, alizungumza na viongozi wa Tazara na kuwataka kuwasilisha mapendekezo yao juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kuboresha usafirishaji wa mizigo na abiria kupitia reli hiyo.

Rais Magufuli alisema serikali inatambua umuhimu wa Tazara na haiwezi kuiacha ikifanya kazi kwa ufanisi mdogo usiowaletea manufaa Watanzania kama ilivyokusudiwa.

Reli hiyo iliyojengwa kwa msaada kutoka China, ilianza kutoa huduma mwaka 1975 na inamilikiwa kwa ubia wa asilimia 50 kwa 50 wa nchi ya Tanzania na Zambia.

Ina urefu wa Km 1,860 ikiwa na uwezo wa kusafirisha tani milioni tano za mizigo kwa mwaka lakini kutokana na uwekezaji mdogo uliosababisha upungufu mkubwa wa injini na mabehewa, inasafirisha chini ya tani 300,000 kwa mwaka.

Mkurugenzi Mkuu wa Tazara, Bruno Chingandu na Meneja Mkuu wa Tazara Tanzania, Fuad Abdallah, walimweleza Rais Magufuli kuwa tayari mapendekezo ya mabadiliko ya sheria yamewasilishwa serikalini ili kuwezesha kila nchi kuwekeza katika Tazara kwa lengo la kuboresha usafirishaji wa abiria na mizigo.

Rais Magufuli aliagiza mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria hiyo uharakishwe ili juhudi za kununua injini na mabehewa zifanyike haraka.

NSSF yawatangazia kiama waajiri wakaidi

Na Salome Kitomari

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umesema wiki ijayo utaanza kupita kwa waajiri nchi nzima ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wasioandikisha na kupeleka michango kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati wa ufunguzi wa semina na uzinduzi wa huduma ya NSSF na marafiki, Mkurugenzi Mkuu wa mfuko huo, Willium Erio, alisema kampeni hiyo itaanza mara moja kwa lengo la kutekeleza sheria.

Alisema utafiti wao umebaini wapo waajiri wengi ambao hawajasajili kabisa waajiriwa wao, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

"Tumepata orodha nchi nzima, tutapita ofisi kwa ofisi kuhakikisha wanachama wanapata haki ya kisheria na waajiri wanatimiza wajibu wao kisheria wa kuandikisha wananchama wao," Erio alisema.

"Ni lazima kujiandikisha kwa mujibu wa sheria na kwa kila aliyeajiriwa kuandikishwa na michango yake kupelekwa ni suala la kisheria," alisisitiza.

Alisema NSSF inapenda waajiri na wanachama kutimiza wajibu kisheria ili kunufaika na matakwa ya sheria na kwamba sekta binafsi yote iko chini ya mfuko huo.

"Nitoe rai kwa waajiri wote kokote waliko kutambua kuwa kwa utaratibu wa sasa, ukiondoa waliko serikali na kwenye taasisi ambazo serikali ina zadi ya asilimia 30 ya hisa, wako chini ya NSSF na wanastahili kupelekewa michango yao," alisema.

Alisema kwa walioajiriwa serikalini na taasisi mbalimbali wanatakiwa kuandikishwa kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Erio pia alisema NSSF imeanzisha utaratibu wa uchangiaji kwa hiyari na kwamba umesajiliwa mfumo wa hiyari ambao walioajiri walio sekta binafsi watapeleka michango yao.

"Tumekamilisha kusajili kwenye mamlaka husika, tutafuata hatua mbalimbali ikiwamo kupeleka michango kwa njia ya simu. Tunazungumza na kampuni za simu ili wanachama waweze kutuma michango yao kwa simu na kupata taarifa," alisema.

Alisema walio kwenye kampuni au taasisi, michango yao inafikishwa NSSF kupitia mfumo wa malipo serikalini ambao hupewa namba maalum ya malipo na kwamba watu binafsi hawawezi kupewa namba hizo na ndiyo maana wanatengeneza utaratibu wao wa kulipa kwa simu.

Erio alibainisha kuwa kundi hilo litanufaika na mikopo itakayotolewa kupitia benki zenye utaalamu na nguvu kazi iliyobobea.

Alisema wako kwenye hatua za mazungumzo na taasisi za fedha ikiwamo Benki ya Posta ili kutoa mikopo na vitendea kazi kwa ajili ya kutanua kazi zao.

Aliongeza kuwa wanachama hao pia watapata huduma za matibabu kwa kuwa wanakamilisha mazungumzo na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ili kutoa bima hizo kwa wanachama hao.

Mkurugenzi huyo alisema mipango yote hiyo inatarajiwa kukamilika na kuanza kazi mwezi ujao.

HABARI KITAIFA

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Vijana, Antony Mavunde (wa pili kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni nne kwa Alphonce Philipo wa Shule ya Msingi Jenerali Musuguri, aliyeibuka mshindi wa kwanza wa shindano la michoro ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule za msingi mwaka 2019, mkoa wa Dodoma jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, waandaaji wa shindano hilo, Dominic Dhanah. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Ushahidi wa video kesi ya kina Mbowe watinga kortini

Na Hellen Mwango

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepokea kamera ya video na tepu rekoda mbili kama vielelezo katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti wake wa Taifa, Freeman Mbowe na wenzake wanane.

Mahakama ilikubali kupokea vielelezo hivyo namba nne na tano, baada ya kutupilia mbali pingamizi la awali la upande wa utetezi kwamba shahidi hajakidhi vigezo vya kutoa vielelezo hivyo.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Alisema kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha sheria ya kielektroniki kimeweka vigezo vya upokeaji wa vielelezo vya elektroniki.

"Shahidi wa sita wa Jamhuri, Koplo Charles, amekidhi vigezo hivyo, mahakama yangu imekubali kupokea kamera moja kama kielelezo namba nne na tepu rekoda mbili kama kielelezo namba tano cha upande wa Jamhuri na inatupilia mbali pingamizi la utetezi," alisema Hakimu Simba katika uamuzi wake.

Alisema kesi hiyo itaendelea leo kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri.

Awali wakili wa utetezi, Peter Kibatala alipinga kupokelewa kielelezo hicho kwamba ushahidi wa kielektroniki hauwezi kupokelewa mahakamani mpaka kuwapo kiapo mahususi kuhusu vielelezo hivyo.

Awali, shahidi wa sita, Koplo Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, alidai kuwa alikimbilia kwenye

INAENDELEA UK. 8

TRA yakamata mashine kukwepa kodi mil. 300/-

Na Gwamaka Alipipi

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imekamata mashine za michezo ya kamari 250 ambazo ziliingizwa nchini kwa njia ya udanganyifu, kuikosesha serikali kodi ya Sh. milioni 300 kwa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari bada ya kuzikamata mashine hizo, Kaimu Meneja TRA Mkoa wa Kikodi Ilala, Stephen Kauzeni, alisema mashine hizo ziliingizwa nchini kama vifaa vitakavyotumika kutengeneza mashine.

Alisema mmliki wa mshine hizo ni Imtiaz Abdulaziz Bandari, ambaye namba yake ya utambulisho wa mfanyabiashara (TIN) ni mkoani Mbeya, lakini taarifa zake zimeonyesha aliacha kufanya biashara mwaka 2014. Kauzeni alisema jina la kibiashara alilojisajili nalo mfanyabiashara huyo ni Bahati Jackpot. "Hizi mashine ziliingizwa kama vifaa vitakavyotumika kutengeneza mashine, lakini ukweli ni kuwa walikuwa na dhumuni na kuziunganisha na kuwa mashine kisha waziingize katika soko," alisema Kauzeni.

Alieleza kuwa mfanyabiashara huyo alishirikiana na kampuni ya China kuingiza mashine hizo kwa makubaliano ya kushirikiana kufanya biashara.

"Endapo mashine hizi zingeingia kwenye soko zingeipotezea serikali kodi ya Sh.milioni 25 kwa kila mwezi, kwa mwaka Sh. milioni 300, lakini tumeziwahi na tumezizuia," alisema Kauzeni.

Alisema baada ya kuzikamata mashine hizo watazizuia kwa sheria ya ushuru wakati sheria zaidi zikichukuliwa.

"Zoezi hili ni endelevu, tunaendelea nalo, tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema. Tumeshaongea na watu wetu wa ushuru ili wawe makini na mashine hizi, tatizo vifaa vinavyotumika katika mashine hizi hazina tofauti na zile zinazotumika katika kompyuta, hivyo ni vigumu kubaini wakati mfanyabiashara anapopeleka nyaraka zake," alisema Kauzeni.

Naye Meneja Ukaguzi na Udhibiti wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Sadiki Elimsu, alisema mashine hizo hazikufuata taratibu wakati wa kuziagiza.

"Mashine kama hizi haziwezi kuingia nchini bila ya kupata kibali kutoa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, kubaini kama bidhaa hizi zinafaa au hazifai. Jukumu letu ni kuwalinda wateja," alisema Elimsu.

Alisema mwagizaji lazima apate leseni kutoka GBT, atapaswa kuleta cheti kutoka maabara kinachoonyesha mashine zimepimwa na zinakidhi viwango kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Alisema lazima mwagizaji aonyeshe kibali bandarini kuwa mshine zake zimekaguliwa na GBT, aonyeshe sehemu anapokwenda kuziweka ambapo bodi itakwenda kukagua eneo hilo kama ni salama.

JKCI yatibu moyo bila upasuaji

Na Mary Geofrey

KWA mara ya kwanza Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Madaktari Bingwa wa China, imefanikiwa kufanya upasuaji wa kuingiza vifaa ndani ya moyo na kuunguza sehemu ambazo zinafanya moyo uende mbio (SBT).

Huduma hiyo ambayo inatolewa kwa wagonjwa wanaotibiwa kwa bima ya afya, fedha taslimu na wenye msamaha, itawezesha wagonjwa wengi waliokuwa hawapati huduma hiyo nchini kunufaika.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alieleza hayo jana wakati akipokea msaada wa fedha kwa ajili ya upasuaji wa watoto 17 ambao hawana uwezo, uliotolewa na wadau waliotafutwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.

Prof. Janabi alisema juzi walimfanyia upasuaji mgonjwa mmoja kwa mafanikio makubwa na lengo ni kufanya upasuaji kwa wagonjwa sita hadi 10 kwa wiki moja.

"Kwa mara ya kwanza Tanzania jana (juzi), tumefanikiwa kufanya upasuaji wa kuingia ndani ya moyo na kuunguza sehemu ambazo zinaufanya moyo uende mbio kwa lugha ya kigeni ni SBT na mgonjwa ametoka salama na sasa yupo wodini anaendelea vizuri kabisa, leo (jana), tayari tumeshaandaa mgonjwa mwingine kwa ajili ya kumfanyia upasuaji," Prof. Janabi alisema.

Awali wagonjwa wenye tatizo hilo walikuwa wanapewa vidonge vya kutuliza maumivu na mapigo ya moyo, lakini haikuwa tiba ya kudumu kama inavyofanyika sasa.

Alisema duniani kote wanatoa matibabu ya aina hiyo ambayo hayana tiba mbadala na kwamba tayari JKCI wana kifaa na miundombinu ya kutoa tiba hiyo na wanachofanya sasa ni kupata utaalamu kutoka kwa madaktari wa China.

"Njia pekee inayotumika duniani ni kuunguza sehemu hiyo hakuna tiba mbadala. Tatizo hilo ni mfano wa sehemu tano au sita ambazo zinatoa umeme kwenye moyo wakati inayotakiwa kutoa umeme ni sehemu moja ili moyo uende sawa, hivyo tunachofanya ni kuunguza sehemu zote ambazo hazitakiwi kutoa umeme na tumerudisha ile sehemu moja inayotakiwa kutoa umeme," Prof. Janabi alifafanua.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo ina idadi kubwa ya wagonjwa wenye tatizo hilo na wanaendelea kuwapatia matibabu hata timu ya madaktari wa China itakapoondoka nchini.

INAENDELEA UK. 8

TANGAZO

AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

		Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-19	Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mar-19
A	**MALI**		
1	Fedha Taslimu	3,705	3,835
2	Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania	7,367	9,523
3	Uwekezaji Katika Amana za Serikali	32,774	34,575
4	Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha	4,452	6,685
5	Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa	190	1
6	Miamala Baina ya Matawi	-	-
7	Bili Zilizoafikiwa	-	-
8	Dhima za Wateja Zilizokubalika	-	-
9	Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine	94,037	88,118
10	Uwekezaji Katika Amana Nyingine	-	-
11	Mikopo Halisi Iliyopo	132,226	135,036
		-	-
12	Mali Nyingine	34,172	33,437
13	Uwekezaji wa Hisa	1,000	1,000
14	Akaunti za udhamini	-	-
15	Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa	4,391	4,486
16	**JUMLA YA MALI**	**314,314**	**316,696**
B	**DHIMA**		
17	Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha	97,633	95,814
18	Amana za Wateja	89,299	97,924
19	Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu	-	-
20	Amana Maalumu	-	-
21	Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha	-	-
22	Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa	-	-
23	Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa	-	-
24	Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja	-	-
25	Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi	-	-
26	Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae	50	38
27	Dhima Nyingine	6,303	3,792
28	Madeni	67,881	65,144
29	**JUMLA YA DHIMA**	**261,165**	**262,712**
30	**MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)**	**53,149**	**53,985**
C	**FEDHA ZA WANAHISA**		
31	Mtaji wa Hisa Uliolipwa	116,014	116,014
32	Akiba ya Mtaji	1,284	1,284
33	Mapato Yaliyobakizwa	(63,123)	(63,123)
34	Faida (Hasara) ya Kipindi Husika	(2,091) -	1,255
35	Akaunti Nyingine za Mtaji	1,065	1,065
36	Stahiki ya Wenyehisa Chache	-	-
37	**JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA**	**53,149**	**53,985**
		(0)	0
38	Dhima Zisizo Dhahiri	8,130	8,214
39	Mikopo Chechefu	22,303	20,245
40	Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu	19,807	17,783
41	Mali Nyingine Chechefu	-	-
D	**BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA**		
(I)	Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali	16.9%	20.0%
(ii)	Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi	14.8%	13.2%
(iii)	Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana	81.3%	78.8%
(iv)	Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi	42.1%	42.6%
(v)	Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali	83.8%	55.7%
(vi)	Ongezeko la Amana	-3.5%	-3.1%
(vii)	Ongezeko la Mali	-0.8%	-1.2%

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

		Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-19	Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Jun-18	Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-19	Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-18
1	Mapato ya Riba	10,765	13,307	21,187	27,291
2	Gharama za Riba	(4,679)	(5,743)	(9,453)	(12,140)
3	**Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)**	**6,086**	**7,564**	**11,734**	**15,151**
4	Madeni Viza Yaliyofutwa/ Yaliorejeshwa	534	-	1,096	-
5	Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo	(719)	(5,288)	(1,454)	(6,297)
6	**Mapato Yasiyo ya Riba:**	**1,324**	**1,319**	**2,617**	**2,514**
6.1	6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni	532	390	999	721
6.2	6.2 Ada na Kamisheni	713	299	1,377	499
	6.3 Gawio	-	-	-	-
6.3	6.4 Mapato Mengine	79	630	241	1,294
7	**Gharama Zisizo za Riba:**	**(8,014)**	**(7,919)**	**(15,992)**	**(15,264)**
	7.1 Mishahara na Mafao	(2,792)	(2,591)	(5,327)	(5,114)
	7.2 Ada na Kamisheni	-	-	-	-
	7.3 Gharama Nyingine	(5,222)	(5,328)	(10,665)	(10,150)
8	**Faida /(Hasara) ya Uendeshaji**	**(790)**	**(4,324)**	**(1,999)**	**(3,896)**
9	Tengo la Kodi ya Mapato	(45)	81	(91)	(48)
10	**Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato**	**(835)**	**(4,243)**	**(2,090)**	**(3,944)**
11	Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)	-	-	-	-
12	**Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka**	**(835)**	**(4,243)**	**(2,090)**	**(3,944)**
13	Idadi ya Waajiriwa	160	157	160	157
14	Mapato kwa Hisa	(0.34)	(1.73)	(0.21)	(0.40)
15		-	-	-	-
16	Idadi ya Matawi	7	7	7	7
	BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI				
(I)	Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali	-0.53%	-4.50%	-1.32%	-2.09%
(ii)	Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa	-3.12%	-24.78%	-7.80%	-11.51%
(iii)	Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi	108.15%	89.15%	111.43%	86.40%
(iv)	Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha	1.76%	3.03%	3.39%	3.03%

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

		Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-19	Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-19
I	**Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:**		
	Mapato/(Hasara) Halisi	(790)	(1,209)
	Marekebisho kwa Ajili ya:	-	-
	- Hasara Katika Mali	1,560	1,559
	- Badiliko Halisi Katika Mikopo	1,463	48,739
	- Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali	-	-
	- Mabadiliko Halisi Katika Amana	(6,807)	(6,183)
	- Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa	1,801	6,034
	- Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine	2,522	(1,570)
	-Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine	(923)	(12,096)
	- Kodi Iliyolipwa	-	-
	- Mengineyo (bainisha)	-	-
	Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji	**(1,173)**	**35,273**
II	**Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:**	-	-
	Gawio Lililopokewa	-	-
	Ununuzi wa Mali za Kudumu	(163)	(362)
	Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu	-	-
	Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala	-	-
	Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala	-	-
	Mengineyo (bainisha)	-	-
	Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji	**(163)**	**(362)**
III	**Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:**		
	Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu	-	-
	Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu	2,738	469
	Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa	-	-
	Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu	-	-
	Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine	-	-
	Mengineyo (bainisha)	-	-
	Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha	**2,738**	**469**
		-	-
IV	**Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:**	-	-
	Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu	1,401	35,381
	Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka	108,161	72,780
	Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka	**109,562**	**108,161**

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 JUNI 2019

	Mtaji wa Hisa	Malipo juu ya bei ya hisa	Mapato Yaliyobakizwa	Ziada ya Kisheria	Tengo la Ziada ya Jumla	Mengineyo	Jumla
Mwaka wa sasa							
Salio la mwanzo wa mwaka	**116,014**	**-**	**(67,756)**	**0**	**1,284**	**1,065**	**50,607**
Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato	-	-	(2,090)	-	-	-	**(2,090)**
Hisa za upendeleo	-						
Mapato mengine yaliyojumuishwa	-	-	-	-	-	-	-
Miamala na wanahisa	-	-	-	-	-	-	-
Gawio lililolipwa	-	-	-	-	-	-	-
Ziada ya Kisheria	-	-	-	-	-	-	-
Tengo la Ziada ya Jumla	-	-	4,633	-	-	-	**4,633**
Mengineyo	-	-	-	-	-	-	-
Salio la mwisho wa mwaka	**116,014**	**-**	**(65,213)**	**0**	**1,284**	**1,065**	**53,150**
	-	-	-	-	-	-	-
Mwaka Uliopita							
Salio la mwanzo wa mwaka	**116,014**	**-**	**(69,349)**	**9,118.58**	**1,114**	**1,384**	**58,282**
Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato	-	-	(7,355)	-	-	-	**(7,355)**
Hisa za upendeleo	-	-	-	-	-	-	
Mapato mengine yaliyojumuishwa	-	-	-	-	-	-	-
Miamala na wanahisa	-	-	-	-	-	-	-
Gawio lililolipwa	-	-	-	-	-	-	-
Ziada ya Kisheria	-	-	9,118	(9,118)	-	-	-
Tengo la Ziada ya Jumla	-	-	(170)	-	170	-	-
Mengineyo	-	-	-	-	-	(320)	**(320)**
Salio la mwisho wa mwaka	**116,014**	**-**	**(67,756)**	**0**	**1,284**	**1,065**	**50,607**

	Jina	Sahihi	Tarehe
Ofisa Mtendaji Mkuu	I. John		26-Jul-19
Mkuu wa Fedha	H. Kandi		26-Jul-19
Mkaguzi Mkuu wa Ndani	J. Kilato		26-Jul-19

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

	Jina	Sahihi	Tarehe
1 Mkurugenzi	Dr J P. Kipokola		26-Jul-19
2 Mkurugenzi	Mr. R. Dave		26-Jul-19

215342502

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

TARIFF

	PRICING (TZS)	PRICING (US $ / EUR)	PRICING GBP
PERSONAL BANKING			
SAVINGS ACCOUNT			
[illegible]			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Monthly Service Fee	Free	Free	Free

MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	$50.00	£50.00
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Monthly Service Fee (1 free withdrawal per quarter)	Free	Free	Free
Extra fee for more than 1 withdrawal per quarter	TZS 1,000.00	$2.00	£2.00

[illegible] SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)			
Account Opening Fee	Free	Free	N/A
Opening Balance	Free	Free	N/A
Minimum Operating Balance	Nil	Nil	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	$25.00	N/A
Monthly Service Fee*	Free	Free	N/A

CURRENT ACCOUNT			
[illegible]			
Account Opening Fee	Free	N/A	N/A
Opening Balance	TZS [illegible]	N/A	N/A
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	N/A	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	N/A	N/A	N/A
Monthly Service Fee*	Free	N/A	N/A

[illegible]			
Account Opening Fee	Free	Free	N/A
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Monthly Service Fee*	TZS [illegible]	[illegible]	N/A

PREMIUM			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Operating Balance	Nil	Nil	Nil
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Monthly Service Fee*	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]

SME BANKING			
[illegible] BIZ ACCOUNTS			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Interest Bearing Balance	[illegible]	[illegible]	[illegible]
Monthly Service Fee*	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]

[illegible] CURRENT ACCOUNTS			
Account Opening Fee	Free	N/A	N/A
Opening Balance	FREE	N/A	N/A
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	N/A	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	Based on the average balance for the month [illegible]		
Monthly Service Fee*	Free	N/A	N/A

SME TIERED INTEREST ACCOUNT			
Account Opening Fee	Free	Free	N/A
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Monthly Service Fee*	TZS [illegible]	[illegible]	N/A

CORPORATE BANKING			
CORPORATE CURRENT ACCOUNTS			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Operating Balance	Nil	Nil	Nil
Minimum Interest Bearing Balance	Nil	Nil	Nil
Monthly Service Fee*	TZS 25,000.00	$20.00	£15.00

CORPORATE CALL ACCOUNTS			
Account Opening Fee	Free	Free	Free
Opening Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Operating Balance	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Minimum Interest Bearing Balance	Nil	Nil	Nil
Monthly Service Fee*	TZS 25,000.00	$20.00	£15.00

CORPORATE TERM DEPOSIT ACCOUNT			
Account Opening Fee	Free	Free	N/A
Opening Balance	[illegible]	[illegible]	N/A
Minimum Operating Balance	NIL	NIL	N/A
Minimum Interest Bearing Balance	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
Monthly Service Fee*	25,000	$25	N/A

GENERAL CHARGES			
Banker's Cheque	TZS [illegible]	[illegible]	N/A

DISHONOURED/UNPAID CHEQUE			
[illegible]	TZS [illegible]	[illegible]	N/A
[illegible]	TZS [illegible]	[illegible]	N/A

Cheque Book Processing Fee			
[illegible] leaves	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
[illegible] leaves	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
[illegible] leaves	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Uncollected cheque book after 3 months	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
3rd party acquirement (with 3rd party [illegible])	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Stop Payment Charges	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]

[illegible]			
Withdrawals via Standing Orders			
Standing Order - Internal (own customer) [illegible]	Free	Free	Free
Standing Order - Internal other customers [illegible]	Free	Free	Free
Standing Order - Other local bank	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Amendment	Free	Free	Free

[illegible]			
Cash Deposit at Branch	Free	Free	Free
Cash Deposit at Branch small denominations [illegible]	[illegible]	[illegible]	N/A
Cash Deposit at Branch small denominations [illegible]	[illegible]	[illegible]	N/A
Cash Deposit at Branch [illegible]	[illegible]	N/A	N/A
With Account Transfers [illegible]	N/A	N/A	N/A
Cheque deposit	Free	Free	Free
Cash withdrawal Personal Banking [illegible]	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Cash withdrawal Personal Banking [illegible]	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Cash withdrawal Personal Banking [illegible]	[illegible]	[illegible]	[illegible]
Cash withdrawal SME [illegible]	[illegible]	[illegible]	[illegible]
Cash withdrawal Corporate Banking	[illegible]	[illegible]	[illegible]
Deposit charges - Financial Institution	Free	Free	Free
Deposit charges - Financial Institution (small denominations)	Free	[illegible]	[illegible]
Account Closure	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Dormant Account Reactivation	Free	Free	Free
Dormant Account monthly fee	TZS [illegible]	[illegible]	[illegible]
Premature/cancelled fixed deposit fee	[illegible]	[illegible]	[illegible]

Monthly statements	Free	Free	Free
Interim Statements (per page)	TZS 2,000.00	$1.00	£1.00
Search fee documents (after 3 months)	TZS 85,000.00	$40.00	£40.00
Audit confirmation	TZS 75,000.00	$50.00	£50.00
Balance Certificate	TZS 50,000.00	$30.00	£30.00
Reference Letter	TZS 50,000.00	$30.00	£30.00
Inter Account Transfers	Free	Free	Free
T T Outward local - TISS	TZS [illegible]	$[illegible]	N/A
T T Outward local - EFT	TZS [illegible]	N/A	N/A
T T Inward local TISS	Free	Free	N/A
Salary processing (per entry)	TZS [illegible]	$1.00	£1.00
International Outward T T	N/A	[illegible] 0.25% Min 50 Max 100	[illegible] 0.25% min 50 max 100+Other overseas bank charges [illegible]
International Inward T T	N/A	Free	Free
Travellers Chq. Deposit	N/A	N/A	N/A
Foreign Banddrafts	N/A	$30.00	£30.00
Outward Cheque for Collection	N/A	N/A	N/A
Outward Bills for collection	N/A	0.25% min 50 + $ 50 (courier charge)	0.25% min 50 + $ 50 (courier charge)
Inward Bills for Collection	N/A	0.25% MIN 50	0.25% MIN 50
Advising fee (inward Bill & LCs)	N/A	$200.00	£200.00
Travellers Chq. Issue	N/A	N/A	N/A
Letters of Credit	N/A	[illegible]% per qtr + $ 50 (total min $250)	[illegible]% per qtr + $ 50 (total min $250)
Bank Guarantees	[illegible]% Per Qtr Min $ 200	[illegible]% per qtr min $200	[illegible]% per qtr min $200

Mobile Banking Prices

Utility Payments

Biller	Description	Commission
Prepaid Airtime	Prepaid recharge for Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel, Smart	Free
Luku	Prepaid electricity	Free
DAWASCO	Water and sewerage bill payment	Free
TTCL	Prepaid voice/data recharge vouchers	Free
StarTimes	Television subscription payment	Free
Precision Air	Flight fare payment	As per B2W tariff
Smile 4G	LTE Internet Service	Free
DSTV	Television subscription payment	As per B2W tariff
IDE Services	Private apartment prepaid electricity payment	Free
Zuku	Television subscription payment	As per B2W tariff
Inter bank	Funds transfer between Selcom managed banks	As per B2W tariff
Bank2Agent	Fund transfer to agents	As per B2W tariff
Azam TV	Television subscription payment	Free
Tanesco Postpaid	Postpaid electricity bill payment	As per B2W tariff
NHC	National Housing Corporation rent payment	As per B2W tariff
Morogoro Municipality	Municipality business tax payment	As per B2W tariff
Bank2Wallet	Funds transfer to Mpesa, Tigo Pesa, Airtel Money, Ezy Pesa, Selcom Paypoint Card, Selcom Castpoint	As per B2W tariff
Wallet2Bank	Funds transfer from Mpesa, Tigo Pesa, Airtel Money, Ezy Pesa, Selcom Paypoint Card, Selcom Castpoint	Free

Dial "*150*34# to access this service		Tariff
100	999	50
1,000	1,999	250
3,000	4,999	400
5,000	9,999	500
10,000	19,999	700
20,000	49,999	1,000
50,000	99,999	1,500
100,000	199,999	1,800
200,000	299,999	2,300
300,000	399,999	2,800
400,000	499,999	3,100
500,000	1,000,000	3,600
1,000,001	3,000,000	3,900
3,000,001		4,300
Bulk mobile payments	TZS 500 per transaction	

Other types of transfers

Balance Inquiry	USSD	APP
	100	Free
Mini Statement Request	USSD	APP
	100	Free
[illegible]	[illegible]	
Account activity alert	Free	
[illegible]	[illegible]	
Local transfer inter bank	3,000	

[illegible] VISA CARDS CHARGES

[illegible]

CONTACTS OF BRANCHES

HEAD OFFICE
+255 22 211[illegible]
+255 22 2 [illegible]
+255 22 2 [illegible]

[illegible] BRANCH
+255 22 2 [illegible]
+255 22 2 [illegible]

QUALITY CENTRE BRANCH
+255 0779 000 [illegible]

ARUSHA BRANCH
+255 27 [illegible]

KARIAKOO BRANCH
+255 779 000 [illegible]

MWANZA BRANCH
+255 779 000 [illegible]

[illegible] BRANCH
+255 [illegible]

CUSTOMER CARE
Mobile Number: 0778 [illegible]
Email: customercare[illegible]
bancabc.com

215342502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

SADC iongeze ari ya usafi Dar

DUNIA ya leo usafi ni jambo linalohitajiwa na kila mtu, aidha pamoja na sababu za kimazingira na kiafya usafi ni njia moja wapo ya kuvutia uwekezaji, watalii na hata mikutano ya kimataifa.

Hili ni muhimu wakati huu Dar es Salaam ikijiandaa na maonyesho na Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Wakuu wa nchi na viongozi wa mataifa 16 ya SADC wanakutana hapa nchini na jambo ambalo ni muhimu kuzikumbusha mamlaka za jiji kuwa na Dar safi.

Usimamizi mbovu wa takataka, unaosababisha malundo ya taka pembeni ya barabara, nyingine kujaa ndani ya mifereji na mitaro, uchafuzi wa hali ya hewa unaosababishwa na harufu mbaya ya taka za samaki huko Feri ni mambo ambayo yanaishushia hadhi Dar.

Ni lazima kukumbuka kuwa sababu za kiafya, zinalilazimisha jiji kuwa safi. Usafi unawaletea watu furaha na amani ya kula , kunywa na kutembea popote kwa sababu hawana hofu ya kupata magonjwa.

Ndiyo maana tunapenda kuwakumbusha 'mababa' wa jiji kuwa jambo la kuzoa taka linaweza kufanyika bila msaada wa wahisani.

Hili linaweza kufanyika kwa kuhakikisha kuwa mazingira tunayoishi kuanzia nyumbani, uwanjani na barabarani tunapotembea ni masafi.

Tunakumbusha usafi kwa sababu tusikitishwa kuona kwamba Watanzania wengi wanashindwa kutupa takataka hata kwenye mapipa ya uchafu.

Ukifika kwenye vituo vya mabasi, hospitalini, shuleni, migahawani na sokoni takataka zipo chini na zinazunguka mapipa ya taka badala ya uchafu kuwekwa ndani ya vyombo hivyo.

Kwanini tatizo hili limekuwa ni la miaka mingi na halina dawa? Inamaanisha watu hawafahamu matumizi ya mapipa hayo?

Tatizo hili linakuzwa na ukweli kuwa watu wetu hawajui kuwa ni wajibu wao kuufanya mji ama makazi yao na mazingira yao kuwa safi. Ni lazima maofisa afya wasaidie kubadili mienendo hii.

Usafi ni wa kila kitu na pengine ndiyo njia ya kumfikia Mungu Muumba. Pengine hii inafaa kuwa nukuu inayotumiwa na wazazi, walezi, walimu na kila mmoja ili kudhibiti uchafu mijini na mitaani.

Tunaona kuwa wakati umefika kwa mamlaka za jiji kuhimiza usafi wakati huu tunapoelekea kwenye mkutano wa SADC na maonyesho ya kiuchumi yanayotarajiwa kufanyika Dar es Salaam mwezi ujao.

Ikumbukwe kuwa usafi ndiyo njia pekee ya kukifanya kisichojulikana kufahamika.

Mathalani, kuwa na Mlima Kilimanjaro mrefu kuliko yote Afrika ni suala la kujivunia sana lakini kuwa na mji msafi sana wa Moshi watu wanapoingia kwanza kabla ya kuupanda Mlima Kilimanjaro na kitu muhimu cha kuuongezea thamani mlima huo.

Ni lazima kuuweka mji kwenye hali ya usafi kuuongezea thamani ya kile ambacho kipo . Dar kuna fukwe nzuri, bahari ya Hindi, Visiwa vya Mbudya na utamaduni wa aina mbalimbali.

Lakini kama mji ukiwa msafi thamani yake inapanda zaidi na umaarufu wake unaongezeka. Pamoja na amani, utulivu, vivutio vingi na miundombinu ya kisasa bila usafi Dar inakosa heshima.

Usafi huvutia watalii, huleta furaha, burudani na kujiamini. Ndiyo maana tunasema SADC iongeze chachu ya usafi Dar.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

Mhariri Mtendaji : Beatrice Bandawe
Meneja Usambazaji na Masoko: Emmanuel Lyimo, 0716 500500
Mapokezi: 0745 700710
Meneja Matangazo: Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
Website: www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

Muungwana Lazima Nilonge

Na Yasmine Protace

Mkakati unaomwepusha mtoto ukatili uanzie ngazi ya familia

MIKAKATI ya kumlinda mtoto dhidi ya matukio ya kingono, kuna kila sababu ya jamii kushiriki kutoa ushirikiano.

Kama jamii itatoa ushirikiano kwa vyombo husika juu ya matukio ya kingono, hapana shaka matukio hayo yanaweza kumalizika kirahisi

Hivi karibuni wadau wa semina za jinsia na maendeleo iliyoandaliwa na asasi ya GNP Mtandao, walizungumzia mikakati ya kumlinda mtoto dhidi ya ukatili uliopo wa kingono.

Kupitia semina hiyo, wadau washiriki walitoa maoni yao namna ya kumlinda mtoto dhidi ya ukatili wa kingono unaoendelea katika jamii.

Pelis Charles, ni kati ya wadau wa GDSS anayesema kuwa, wazazi wanatakiwa kufuatilia mienendo ya watoto watokapo shule na nje ya hapo.

Anasema kuwa wazazi, hata wanapokuwa katika baadhi ya shughuli zao kama mjumuiko wa vikoba, wanapaswa kujadili masuala ya ukatili na kamwe, sio kujadili masuala ya pesa.

Charles, anaongeza kuwa wazazi mara zote wanapaswa kujenga utamaduni wa kuzungumza na watoto wao na kuwaeleza namna ya kujilinda na ukatili wa kingono.

Grace Muhaba ni mwalimu katika shule ya sekondari iliyopo jijini Dar es Salaam, anasema kuwa shuleni kake wanashudia jinsi wanafunzi wanavyolalamika kuhusu ukatili wa kijinsia wanaofanyiwa.

Grace Muhaba ni mwalimu katika shule ya sekondari iliyopo jijini Dar es Salaam, anasema kuwa shuleni kake wanashudia jinsi wanafunzi wanavyolalamika kuhusu ukatili wa kijinsia wanaofanyiwa.

Pia, anaeleza haja ya wazazi kuwachunguza watoto wanaotoka shule, hali kadhalika wasichana waliowaajiri kutumikia majukumu majumbani.

Kwa mujihu wa Grace, sule zilizopo nchini zinapaswa kuwa na katuni na vipeperushi vingi vyenye ujumbe wa kukabili matukio ya ngono katika jamii zao.

Kelvin Godwin, ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Mabibo, anayewashauri wazazi wawe karibu na watoto na wawe wanawachunguza iwapo wameshafanyiwa ukatili wa kingono.

Lingine analoshauri wazazi kuwa marafiki wa watoto wao, ili waweze kuzungumzia kwa uwazi adha za masuala yanayohusu ngono.

Anna Sangai, ni Ofisa wa Programu, Harakati na Ujenzi wa Nguvu za Pamoja wa TGNP Mtandao, anasema kuwa bila elimu ya kijinsia, itakuwa ngumu kwa wanafunzi wa kike kuyafikia malengo yanayowakabili.

Anaongeza kuwa, katika kumlinda mtoto na matukio hayo, TGNP Mtandao imezindua kampeni ya kuwalinda watoto, ikitoa namna maalumu za kuwasiliana nao. Anna, anashauri wazazi kuwa wanapaswa kutumia majumuiko wa siku ya vikoba, kujadili masuala ya jinsia katika mjumuiko wa vikoba na vyema wakaishia kuijadili masuala ya pesa, kabla ya kuacha kuzungumzia yanayohusu ukatili wa kingono kwa watoto.

Amina Juma, ni mdau mwingine anayesema kutolewa elimu kutaisaidia jamii kutoa ushirikiano, pale tatizo litakapotokea anasema kuwa, matukio ya kingono yanapotokea, baadhi ya familia zinamalizana na hali hiyo. Hiyo inasababisha aliyefanyiwa jambo hilo kukosa haki yake.

Anasema, mila na desturi mbovu kwa baadhi ya watu imechangia panapotokea matukio hayo wamekuwa pande zote mbili kumalizana.

Wito wake anasema kuwa vipeperushi visambazwe katika shule ambayo vinaonyesha ujumbe unaozungumzia ukatili.

HABARI KITAIFA

Simbachawene atoa neno kwa NEMC

Na Enock Charles

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, aneeleza kuridhishwa na utendaji wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), na kulitaka kusimamia sheria na taratibu katika kutekeleza majukumu yake ili kufikia malengo ya Taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara yake ya kwanza alipozungumza na uongozi wa baraza hilo jijini Dar es Salaam jana, Simbachawene alisema mbali ya kuridhishwa na kazi za baraza, atategemea kupata ushirikiano mkubwa wa baraza hilo.

"Mimi bado mgeni katika wizara hii hii, hivyo nategemea kujifunza zaidi kutoka kwenu watendaji wa Baraza, hivyo ushirikiano wenu kwangu ndio utaniwezesha kuelewa kwa haraka mambo yote yanayofanywa na baraza hili ili twende sambamba katika utekelezaji wa majukumu," Simbachawene alisema.

Waziri huyo aliyeambatana na Naibu Waziri Waziri wa wizara hiyo, Musa Sima, alisema matumaini yake kwa baraza ni makubwa kutokana na hali na utayari wa watendaji wake katika kutekeleza majukumu yao na kuifanya nchi kubaki katika hali ya mazingira salama na endelevu.

Alisema jukumu la kutunza mazingira ni la kila Mtanzania, hivyo ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi umuhimu wa mazingira na athari zake endapo tahadhari hazitachukuliwa.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, mbali ya kumpongeza kwa kuteuliwa kwake, alimshukuru pia kufanya ziara NEMC na kuahidi kumpa ushirikiano ili aweze kufikia malengo aliyojiwekea.

"Changamoto kubwa inayolikabali baraza ni pamoja na upungufu wa wafanyakazi hali inayochangia ucheleweshaji wa baadhi ya kazi kutokana na mtu mmoja kukabidhiwa miradi mingi ambayo ndani ya muda mfupi inahitajika yote ikamilishwe, hii ndio sababu ya lawama kutoka kwa wawekezaji," Dk. Gwamaka alisema.

Ziara ya Waziri Simbachawene NEMC ni ya kwanza tangu ateuliwe na Rais John Magufuli Jumamosi iliyopita kushika nafasi hiyo iliyokuwa ikishikiliwa na Mbunge wa Bumbuli, January Makamba, ambaye uteuzi wake ulitenguliwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangalia mkaa wa mawe, uliyotengenezwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na wajasiriamali wa kikundi cha Mbalawala Women Group, wakati akikagua mabanda kwenye maonyesho ya viwanda na kongamano la uwekezaji mkoani Ruvuma jana. Kulia ni Meneja wa Fedha wa kikundi hicho, Esta Silas na Msimamizi wa Mradi, Hajra Yakub. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

Uingereza yasaidia ujenzi madarasa nchini bil. 18/-

Na Halima Ikunji, TABORA

SERIKALI ya Uingereza imegharamia ujenzi wa madarasa zaidi ya 700 za shule za msingi katika mikoa tisa ya Tanzania Bara kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 18.

Madarasa hayo mapya yameongeza nafasi za masomo kwa zaidi ya watoto 10,000 na pia ujenzi huo umehusisha vyoo zaidi ya 1,300.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) nchini, Beth Arthy, katika uzinduzi wa kituo cha mafunzo ya awali cha Malole katika Halmashauri ya Nzega, mkoani Tabora.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa ni Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliyefuatana na Kaimu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Tixion Nzunda.

Arthy alisema Malole ni moja ya vituo shikizi vilivyofadhiliwa na Serikali ya Uingereza pamoja na nguvu za wananchi.

Alisema ufadhili wa Serikali ya Uingereza ulipitia katika mradi wa EQUIP-T, ambao pamoja na ujenzi huo wa madarasa na vyoo, mradi huo pia umetoa mafunzo kazini kwa zaidi ya walimu 50,000, walimu wakuu 5,000 na waratibu elimu kata 1,300.

Alisema Mkoa wa Tabora kupitia mradi wa EQUIP-T umejenga madarasa 95, vyoo 176 na ofisi za walimu 32. Pia mradi umetoa mafunzo kwa wakuu wa shule 773 na waratibu elimu kata 206 katika Mkoa wa Tabora na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili."Serikali ya Uingereza inajivunia kuwa mfadhili mkubwa katika sekta ya elimu nchini Tanzania," alisema Beth.

Vile vile, alisema Serikali ya Uingereza imetenga zaidi ya Sh. bilioni 600 ili kugharamia utoaji wa elimu bora ya msingi kwa watoto wa kitanzania.

Pia, aliupongeza Mkoa wa Tabora kwa kuongeza kiwango vya ufaulu katika shule za msingi kutoka asilimia 37 mwaka 2013 hadi asilimia 73 mwaka 2018.

Alisema Serikali ya Uingereza imetenga fedha za kiasi cha Sh. bilioni 600 kwa ajili ya sekta ya elimu kupitia mpango wa EQUIP-T, mradi wa malipo kwa matokeo makubwa (EP4R) na mradi wa elimu kwa watoto wa kike (GEC) na mradi wa GPE (Global Partnership in Education).

Mradi wa EQUIP-T ambao unafadhiliwa na serikali hiyo toka mwaka 2013 na utafika kikomo mwaka 2019.

Mradi huu unaunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania katika kuinua ubora wa elimu ya msingi nchini na kuongeza ufaulu wa watoto wa kike kutoka shule za msingi kwenda shule za sekondari ikiwa ni pamoja na kuinua viwango vya kujifunza, stadi za kusoma, kuhesabu na kuandika (KKK).

Programu hiyo ipo katika mikoa tisa ya Tanzania Bara iliyokuwa na ufaulu mdogo mwaka 2013 ni Kigoma, Katavi, Tabora, Simiyu, Shinyanga, Singida, Mara, Dodoma na Lindi.

Walimu walazimika kuchana khanga kuwahifadhi wanafunzi wa kike hedhi

Na Lilian Lugakingira, MULEBA

WALIMU wa kike wa Shule ya Msingi Kagondo "B" yenye watoto wenye mahitaji maalum, wilayani Muleba mkoani Kagera, wanalazimika kuchana khanga na vitenge vyao ili kuwapatia vitambaa vya kujihifadhi wanafunzi wa kike wenye ulemavu wanapoingia kwenye hedhi.

Akizungumza wakati wa kupokea viti maalum saba (wheel chairs) kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu vilivyotolewa na Shirika la World Vision Tanzania, mradi wa Izigo, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ester Rwamtoga, alidai wazazi wa watoto hao wanapowafikisha shuleni, hawajishughulishi na suala lolote kuhusu watoto wao.

"Tunalazimika kuchana khanga zetu na vitenge ili kuwapatia vipande watoto wa kike wenye ulemavu, na kisha tunawaelekeza wakishavitumia wavifue wavitunze kwa ajili ya kuvitumia wakati mwingine," alisema mwalimu huyo.

Mwalimu Rwamtoga alisema watoto wenye ulemavu wanaanza shule wakiwa na umri mkubwa ndiyo maana wanakuwapo wanafunzi wengi wanaoingia hedhi kabla ya kuhitimu darasa la saba.

Alisema wakati mwingine analazimika kutoa fedha kidogo kutoka katika ruzuku inayotolewa kwa shule hiyo ili kuwanunulia watoto hao khanga na kuwachania kwa ajili ya kujihifadhi.

Kutokana na tatizo hilo wamemshirikisha Diwani wa Kata Muhutwe, Justus Magongo, ili awasaidie kupata taulo za kike kwa ajili ya watoto hao.

"Lakini pia hatuna chumba maalum kwa ajili ya faragha ya wanafunzi hawa, ingawa sasa kuna sehemu tumetenga ndiyo wanaitumia kubadilishia, tunaomba kujengewa bweni kwa ajili ya watoto hawa ambalo inabidi kuwa na chumba maalum cha watoto wa kike kubadilishia vitambaa," alisema.

Mmoja wa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo anayesoma darasa la tatu, Sarah Damasen (18), akizungumza na Nipashe aliomba serikali na wadau kuwajengea bweni karibu na shule ili kuwaondolea adha ya kufuata huduma hiyo mbali na shule.

"Tunapolala ni pafinyu, lakini pia jengo liko mbali kidogo na shule, tunapata shida kutembea kutoka huko kuja madarasani, tunaomba kujengewa bweni karibu na shule ili kutupunguzia usumbufu, maana wakati mwingine tunalazimika kubebwa na wanafunzi wenzetu wasio na ulemavu kutuleta madarasani," alisema.

Ushahidi wa video kesi ya kina Mbowe watinga kortini

INATOKA UK. 3

gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Aidha, alidai mihemko hiyo ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mbowe kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya serikali.

Jopo la Jamhuri liliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Dk. Zainabu Mango, Mawakili wa Serikali Jaqueline Nyantori, Wankyo Simon na Salimu Msemo.

Akiongozwa na Wakili Kadushi, shahidi alidai Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kufanya kavereji ya mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video, ilipofika saa 10 alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani nilimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali," alidai na kuongeza:

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera."

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vincent Mashinji, Mbunge wa Iringa Mjini, Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Zoezi la kusajili taasisi chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 3/2019, ambayo awali yalisajiliwa chini ya sheria nyingine, likiendelea kwa Kanda ya Kati kwenye ukumbi wa Mwalimu J.K. Nyerere wa Chuo cha Mipango Dodoma, jana. **PICHA: WAMJW**

JKCI yatibu moyo bila upasuaji

INATOKA UK. 3

Vile vile, alisema kuendelea kuwapo kwa teknolojia mpya za kutoa matibabu katika taasisi hiyo, kunapunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi ambayo sasa imefika asilimia 14 wakati asilimia 86 wakipatiwa matibabu nchini.

Kuhusu masaada huo, alimshukuru Makonda kwa kuendelea kuwezesha matibabu ya watoto wasio na uwezo na kuwa mwezi huu wamewafanyia upasuaji watoto 20.

Watoto wengine 17 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji katika msaada uliotolewa na mkuu huyo wa mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo familia ya Mbunge wa Kibaha Vijijini, Silvestry Koka, iliyotoa Sh. milioni 10 na baadhi ya washereheshaji waliotoa mchango wa fedha.

"Tunashukuru kwa msaada huu, kwa kuendelea kusaidia watoto wasio na uwezo walio katika taasisi yetu. Kupitia msaada huu tutaweza kutoa matibabu kwa watoto 17 kati ya 20 ambao tumepanga kuwafanyia upasuaji hivyo taasisi itatafuta msaada wa watoto wengine watatu waliobaki," Prof. Janabi alisema.

Kwa upande wake Makonda, aliwasihi Watanzania na watu wenye mapenzi mema kujitokeza kusaidia watoto hao ili ya kuokoa maisha yao.

Alisema tayari ameahidi kusaidia watoto 60 katika taasisi hiyo kunzia Julai, mwaka huu hadi Desemba na atahakikisha anatimiza lengo hilo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Jukumu langu ni wananchi ninao waongoza na furaha yangu ni wale ninao waongoza na utu unathamani kubwa, nimejitolea kuhakikisha nawasaidia watoto hawa ambao wanatoka mikoa mbalimbali nchini kupata matibabu ya moyo," alisema.

PM atangaza fursa za uwekezaji Ruvuma

Na Beatrice Moses

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amehamasisha wawekezaji kuwekeza mkoani Ruvuma akibainisha kuwa ni kitovu cha uwekezaji kutokana na kuwa na fursa nyingi na miundombinu ya uhakika.

Aliyasema hayo jana, alipokuwa akizindua kongamano la uwekezaji katika viwanda na biashara, lililofanyika kwenye Viwanja vya Majimaji mjini Songea Mkoa wa Ruvuma.

"Mkoa wa Ruvuma una ardhi yenye rutuba, upo kwenye G7 ya mikoa inayozalisha vyakula, pia una uhakika wa umeme, awali walikuwa wanatumia jenereta sasa yamebaki kama makumbusho.

Alisema hali imebadilika katika mkoa huo ambao awali uliyumbayumba kutokana na kukosa barabara za uhakika, hivyo usafiri ulikuwa wa shida.

Alisema sasa Uwanja wa Ndege wa Songea unaendelea kutokana na serikali kutenga Sh. bilioni 37 na kufanikisha hilo.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa serikali imeamua kuwekeza kwenye miundombinu ya barabara, bandari na kwamba uwekezaji hapo hauna shida ya malighafi zitaondoka kwa reli hatua ambayo inafanikisha mkoa huo kufunguka kibiashara.

"Serikali imeamua kuwekeza katika mkoa wa Ruvuma katika fursa mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Tumejipanga kwa uwezeshaji na uwekezaji wakati ni huu wa kufanya maamuzi ya kuwekeza wakati ni huu wa kuwa na mtaji, uwezeshaji unaopigiwa debe," Waziri Mkuu alisema.

Vile vile, alisema umeme umeunganishwa Makambako kwenye gridi kubwa ambayo itaunganishwa na Mtwara, Lindi na Mbeya, ambao utasaidia kuendesha mitambo yoyote ya wawekezaji ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa zao kwa uhakika.

KITUO CHA UWEKEZAJI

Alisema Aprili mwaka huu kipitia kitengo cha uwekezaji wamefungua ofisi ambayo kila mkoa kuwa na Ofisa wa TIC ili awe anaunganisha na kituo cha kanda.

Alisema manispaa kama kitovu cha uwekezaji imetenga maeneo ikiwamo ya mjini kwa shughuli mbalimbali za kilimo na biashara za kawaida.

Tunduru, Namtumbo madini aina ya ulanium yanapatikana hapo na mazao mengine ikiwamo alizeti. Madaba, kunalimwa tangawizi na mahindi kwa wingi, Mbiga, maarufu kwa uzalishaji wa kahawa.

"Bambabey tunahitaji hoteli za nyota tano, nenda kajenge watalii wapo, unaweza kuwekeza kwa kuweka boti za mwendo kasi kwa kutumia ziwa nyasa, pia tunapata madini mengi," alisema.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, alisema mkoa wake una fursa mbalimbali ikiwamo uchimbaji wa madini, makaa ya mawe, samaki wa mapambo ambao ni kivutio kikubwa kwa watalii, pia kuna michoro ya miamba na utamaduni.

HABARI KITAIFA

Vyuo vikuu afya vyajadili kuanzisha mtaala linganifu

Na Mary Geofrey

KATIKA kuboresha sekta ya afya nchini vyuo vikuu vitatu vinavyotoa mafunzo ya afya nchini, vimewakutanisha wadau kwa ajili ya kujadili na kutoa mapendekezo ya kundaa mtaala linganifu itakayowezesha vyuo vyote kuzalisha wahitimu wenye viwango sawa.

Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) haina mtaala wa pamoja wa vyuo vya afya nchini hali inayosababisha kila chuo kuwa na mtaala wake, hivyo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (Muhas), Chuo cha Sayansi ya Afya na Tiba cha Bugando (Cuhas) na Chuo Kikuu cha Afya (KCMC), waliungana kwa pamoja kuandaa mtaala wa pamoja utaowezesha wahitimu bora.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Muhas, Prof. Apolinary Kamuhabwa, akizungumza katika mkutano huo, alisema umewakutanisha wadau wakiwamo vyama vya wanafunzi, wawakilishi wa vyuo vya afya, walimu na TCU kwa lengo la kujadili kwa pamoja na kutoa mapendekezo ya mtaala huo. "Huu ni mwendelezo wa juhudi za taasisi za elimu ya juu katika kuboresha mtaala huu maana hatuna mtaala wa pamoja unaongoza vyuo vya afya vya umma na binafsi ili kutoa wanafunzi wenye taaluma linganifu.

"Tunabadilisha mtaala kwa sababu ya kuwapo kwa magonjwa mapya na kukua kwa teknolojia ili jamii ipate huduma bora kutoka kwa wataalamu wanaotoka katika vyuo vyetu wakiwa na elimu inayokidhi mahitaji," Prof. Kamuhabwa alisema.

Alisema katika vyuo nane vinavyotoa elimu ya afya nchini vinatofautiana mtaala hali inayosababisha wahitimu kuwa na viwango tofauti vya utendaji lakini wakimaliza masomo wanaenda kuhudumia wagonjwa kwa pamoja.

Alisema katika kuandaa mtaala huo wanaangalia vitu muhimu ambavyo daktari anapaswa kuvipata akiwa masomoni ili mtaala utakapokamilika usaidie kupatikana kwa wataalamu wenye vigezo sawa na watakaotoa huduma linganifu.

Naye Mkurugenzi wa Wataalamu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Saitore Laizer, alisema mradi huo utasaidia kupunguza changamoto za sekta ya afya.

Mkurugenzi wa Ithibati wa TCU, Dk. Telamu Kassile, alisema kuwapo kwa mtaala huo utasaidia kuzalisha wahitimu bora watakaoweza kuhudumia sekta ya afya kikamilifu.

Uzinduzi wa mradi huo wa miaka mitano uliofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la JHIEPIGO kwa Dola za Marekani milioni tatu, ulizinduliwa Februari 19 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mafundi wa Kampuni ya Estim, wakiendelea na kazi ya awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Wamiliki wa kumbi za starehe wafunguka mazito kwa NEMC

Na Enock Charles

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wamiliki wa kumbi za starehe, sherehe, disko vilabu vya pombe na baa kuweka vifaa vya kupima na kufuatilia sauti, huku nao wakifunguka mazito.

Lengo ni kuhakikisha sauti zinazotoka katika maeneo hayo hazizidi kiwango kilichoruhusiwa na kanuni za mwaka 2015 za viwango vya udhibiti wa uchafuzi wa kelele na mitetemo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza limekuwa likipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu kero na usumbufu mkubwa wanaoupata kutokana na kelele zinazotoka katika kumbi za starehe, disko, vilabu vya pombe na baa.

"Kila mtu anayeishi Tanzania ana haki ya kuwa na mazingira safi na salama ya kiafya, hivyo ni wajibu wa mmiliki wa mashine, kiwanda, mtambo, baa na kumbi za starehe kutumia njia yoyote iwezekanayo kuthibiti kelele zinazotoka katika eneo lake," Dk. Gwamaka alisema.

Akizungumzia kiwango cha kelele kinachoruhusiwa, alisema kiwango cha juu cha kelele kinachoruhusiwa kwa maeneo ya kumbi za starehe ni dBA60 mchana katika eneo la makazi na dBA40 usiku na katika eneo la biashara ni dBA75 mchana na dBA 50 usiku, katika eneo la viwanda ni dBA 85 mchana na dBA 65 usiku .

Kiwango cha juu cha kelele cha kutangaza kwa kipaza sauti katika eneo la makazi ni dBA 60 mchana na dBA 40 usiku, eneo la biashara ni dBA 75 mchana na 50 usiku na katika eneo la viwanda ni dBA85 mchana na 65usiku.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Kumbi za Baa na Burudani Tanzania (Ubakuta), aliyejitambulisha kwa jina la Mponjoli, alisema kiwango cha umbali wa sauti katika kumbi za starehe kilichowekwa katika kanuni ni kidogo sana, hivyo kuathiri bendi za muziki nchini na kushauri kiwango hicho kiongezwe.

"Changamoto tulionayo sisi wamiliki wa baa na kumbi za starehe ni mahusiano na watu kwa sababu ikipiga kelele kidogo hata ambae hajui sheria analalamika kelele, anayeijua sheria anaenda kushtaki, asilimia kubwa ya wamiliki wa baa tunalalamikiwa, tunatamani wangeongeza huo umbali angalau zifike 85 hizo 60 ni kidogo sana," alisema.

Mmiliki wa baa inayojulikana kama Mikasa Lounge ya Tabata, Dar es Salaam, Allan Hemed, alisema kanuni zilizowekwa zinaweza kutumiwa vibaya na wenyeviti wa Serikali za Mitaa kwa kuzitumia kama njia za kujipatia kipato kutoka kwa wamiliki wa kumbi za baa na starehe.

"Kuna changamoto ya kimahusiano kati ya wenyeviti wa serikali za mitaa, madiwani na viongozi wengine ambao kwa namna moja naona wamepewa nguvu kubwa sana ambayo naamini kuwa itatuumiza sisi kiasi kwamba NEMC ilitakiwa wajipe muda wa kupata maoni ya wadau," Allan alisema

Akijibu hoja za wadau hao, Dk. Gwamaka, alisema baraza hilo halina nia ya kuwakwamisha wafanyabiashara hao kwa kuwa ni walipakodi na kuongeza kuwa lengo ni kuhakikisha kuna kuwa na maelewano baina ya wamiliki wa kumbi za starehe na baa pamoja na watumiaji wengine wa mazingira.

Onyo kali kwa wanunuzi pamba

Na Happy Severine, BARIADI

SERIKALI imetoa onyo kali kwa wanunuzi wa pamba nchini, kwa kushindwa kutekekeza makubaliano ambayo waliwekeana na serikali kuhakikisha wananunua pamba yote ambayo bado ipo kwenye maghala.

Kauli ya serikali imekuja baada ya kuendelea kuwapo kwa pamba nyingi kwenye maghala hayo, wakati serikali iliwadhamini wanunuzi wote kuchukua fedha benki na kuanza kununua pamba.

Onyo hilo lilitolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, baada ya kutembelea na kujionea pamba ikiwa imehifadhiwa nje ya ghala katika chama cha msingi cha ushirika (Amcos) Zuya Mtaa wa Nyakabindi Halmashauri ya Mji Bariadi.

Mgumba alisema wanunuzi wa pamba walikubaliana na serikali wadhaminiwe ili kukopeshwa na benki, jambo ambalo lilifanyika, lakini anashangaa kwa nini mpaka leo wameshindwa kununua pamba.

Alisema serikali ilichukua dhamana hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa pamba na fedha ambazo wanunuzi walikopeshwa na benki zinatakiwa kutumika kwa ajili ya kununua pamba tu.

"Nimewasiliana na benki zote zimewakopesha wanunuzi pesa kwa ajili ya kuja kununua pamba, lakini mpaka leo hawajaanza, niwatake wanunuzi wazingatie makubaliano yao na serikali," alisema Mgumba.

Wilaya ya Ikungi yapata DC mpya

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli amemteua Edward Mpogolo kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, uteuzi huu ulianza juzi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Mpogolo anachukua nafasi ya Miraji Mtaturu ambaye amechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

Kabla ya uteuzi huo, Mpogolo alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma. Nafasi ya Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma itajazwa baadaye.

Waziri aipa majukumu Bodi Mfuko Barabara

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ameivunja Bodi ya Mfuko wa Barabara nchini na kuunda mpya, ambayo itaendesha mfuko huo kwa miaka mitatu ijayo.

Waziri Kamwelwe alifanya uamuzi huo juzi kutokana na kumaliza muda wake. Kwa mujibu wa sheria, wajumbe wa bodi hiyo wanatakiwa kukaa madarakani kwa miaka mitatu na wanaweza kuongezwa kipindi kingine cha miaka mitatu na baada ya hapo wanafikia kikomo.

Baada ya kuunda bodi mpya, Kamwelwe aliiagiza kuhakikisha inasimamia vizuri mfuko huo ikiwamo kuhakikisha miradi yote inayotekelezwa inakuwa na thamani halisi ya fedha zinazotolewa.

Alisema barabara nyingi nchini zinakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa miundombinu yake ikiwamo wizi wa alama za barabarani, umwagaji wa mafuta ambayo yanasababisha ajali na kupitisha mizigo mizito kuzidi uwezo wa barabara.

Aliitaka bodi hiyo kuhakikisha inasimamia vizuri mfuko huo kwa kuhakikisha watu wote wanaoharibu miundombinu ya barabara wanashughulikiwa kama wahujumu uchumi wengine.

"Lakini mbali na hayo naiagiza bodi mpya kazi yenu ya kwanza kwa kushirikiana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi ni kuhakikisha mnaijenga barabara ya mchepuko yenye urefu wa kilomita 40 kutoka Uyole mpaka Songwe kwa kiwango cha changarawe ili malori yapite huko na tupunguze ajali," alisema Kamwelwe. Aidha, aliitaka bodi hiyo kuanza kutekeleza mradi huo katika mwaka wa fedha 2019/2020 na ndani ya mwezi mmoja kuanzia sasa impatie taarifa ya utekelezaji wake.

Katika hatua nyingine, Waziri Kamwelwe alitoa siku 14 kwa Wakala wa Barabara (Tanroads) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi kuwalipa fidia wananchi wa Mji wa Kasumulu wilayani Kyela wanaotakiwa kupisha mradi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Tanzania na Malawi.

Alisema Rais John Magufuli aliagiza wananchi hao walipwe tangu Mei mwaka huu, lakini anashangaa mpaka sasa hawajalipwa licha ya fedha za kuwalipa kuwa tayari zimeshaingizwa kwenye mfuko wa Tanroads.

"Nilitaka niwape siku tatu kuwalipa wananchi hao, lakini kwa sababu ni masuala yanayohusu fedha nawapa mpaka kufikia Agosti 10 muwe mmewalipa wote na atakayekwamisha tutaonana," alisisitiza Mhandisi Kamwelwe.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia ujenzi, Elius Mwakalinga, alisema ameshawatembelea wananchi hao na kuwapa matumaini ya kulipwa fidia hizo.

Homa ya ini tishio kwa Kigoma

Na Romana Mallya

KATI ya watu 6,858 waliopimwa afya kuangalia ugonjwa wa homa ya ini mkoa wa Kigoma kuanzia mwezi Desemba hadi Julai mwaka huu, waliobainika ni 235.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Paul Chaote, akizungumza na moja ya mtandao wa kijamii alisema zipo juhudi ambazo zimefanywa na serikali ikiwa ni pamoja na utolewaji wa chanjo za bure kwa watoto ili kuwakinga.

"Upo utaratibu wa utoaji wa chanzo kwa watu wazima ambao unatolewa kwa uchangiaji wa Sh. 40,000. Elimu inatolewa kwa jamii, watu wazima wanatakiwa kuhakikisha wanapata chanzo na kuepuka kupata maambukizi ya homa ya ini," alisema.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka jana, wateja 5467 waliowapima wakati wakichangia damu kati yao, 374 walionekana kuwa na TCB ikiwa ni asilimia 6.8 na TCC ilikuwa ni asilimia moja.

Alisema ikilinganishwa na idadi ya waliopimwa Ukimwi ni asilimia 1.6 waliokutwa navyo.

"Hapo unaweza kuona maambukizi ya homa ya ini ni makubwa kuliko yanayotokana na ugonjwa wa Ukimwi kwa idadi hiyo hiyo waliyopima watu," alisema.

Alisema watu hao 6,858 waliopimwa, 235 walikutwa na TCB na 80 walikuwa na TCC.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Musilimu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa mkutano kuhusu miundombinu ya usafirishaji salama. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

'Fursa zilizopo baharini ni mabilioni ya fedha'

Na Beatrice Moses

CHAMA cha mabaharia nchini kimebainisha fursa za kiuchumi zilizopo kwenye sekta ya bahari ambazo serikali ikisimamia na kuwezesha utekelezaji wake itavuna mabilioni ya fedha, hivyo kuinua kiwango cha uchumi.

Wamebainisha kwenye sekta ya bahari kuna ajira za nchi kavu na baharini, ambapo ni pamoja na zile zinazohusiana na meli katika bahari kuu na ajira kwenye meli za wavuvi.

Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Josiah Mwakibuja, aliyasema hayo wakati akisoma risala kwenye uzinduzi wa Siku ya Bahari ya Afrika, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza mbele ya mgeni rasmi Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema serikali ikichukua hatua za makusudi za kuwapatia mabaharia wake ajira za uvuvi katika bahari kuu jambo ambalo nchi zingine zinafanya ikiwamo Ufilipino na Indonesia.

"Kuweka mkakati wa ajira kwa mabaharia katika meli za kimataifa nchi yetu itapata mapato makubwa, iwapo itakubaliana na kampuni ya MSC na PIL kuajiri mabaharia wetu 20,000 cheo cha AB(Able Seamen) kwa mshahara wa dola 900 mara 20,000 itafanikiwa kupata Sh. bilioni 479,088,000,000," Mwakibuja alisema.

Alisema pia katika uvuvi wa samaki kwenye habari kuu unaweza kuzalisha viwanda vya kuchakata samaki ikiwamo aina ya Tuna ambao kilo moja inauzwa kwa Dola za Marekani 60.

" Kama meli inaweza kuwa na tani 3,000 ni sawa na kilo milioni 3 ambayo ukifanya 3,000,000 mara 60 ni sawa na dola 180,000,000 ambayo ni meli moja tu, fedha hiyo ikibadilishwa inakuwa sawa na shilingi 399,240,000,000," Mwakabuja alibainisha.

Alisema bahari na mazingira yake yanatoa huduma nzuri kwa mazingira katika Afrika, wakati ambapo Waafrika wengi wanaishi katika hali ya umaskini uliokithiri.

Alibainisha fursa zinazotokana na bahari kwa Waafrika wengi ni na chakula na kipato, kuimarisha hali ya mazingira kwa kunyonya hewa chafu ya CO_2 kutoka angani.

"Vyote hivi katika umoja wake utunyima fursa sisi Tanzania kama nchi maskini tujiulize nchi kama ya Ushelisheli haina madini, ardhi ya kilimo, misitu," Mwakabuja alisema.

Alisema Tanzania inahitaji kujifunza jinsi ya kutumia fursa za kiuchumi zilizopo baharini kutoka katika nchi hiyo ambayo inapakana kwenye bahari na Tanzania.

"Fursa za bahari wanazitua ipasayo tofauti na sisi tunaziangalia tu pale wanapokosa nguvu kazi wanahitaji watu kutoka nje ikiwamo kutoka Kenya, wana viwanda vya minofu ya samaki.

Naibu Waziri Kwandikwa alisema serikali ipo kwenye juhudi za kuinua uchumi kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwamo kupanua Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema serikali inashiriki kikamilifu katika kuhakikisha changamoto zinageuzwa kuwa fursa ili kuwezesha mafanikio kupatikana katika sekta ya bahari.

"Chuo kinazalisha mabaharia, tunaendelea kuunda meli kwa kasi kubwa hivyo tunatarajiwa kuwatumia vyema wataalamu wetu tuliowazalisha kwenye chuo hiki cha bandari," Kwandikwa alisema.

Alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na kongamano la kujadili mawasilisho kutoka kwa wataalamu wa sekta ya bahari, ulinzi, usalama, uchumi, ustawi wa jamii na uchafunzi na utuzwaji wa mazingira katika bahari Afrika. Mrejesho wa huduma zinazotolewa na taasisi zinazohusiana sekta ya bahari.

Mkurugenzi Mkuu Shirika Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, alisema Tanzania haijafanikiwa kutumia vyema fursa zilizopo kwenye sekta ya bahari.

Alisema hali hiyo inachangiwa na kutokuwa na uwezo wa vitendea kazi zikiwamo meli za uvuvi, imesababisha meli kadhaa kutoka nje ya nchi zikiwamo za maharamia kuja kuvua samaki na kufanikiwa kuondoka nao.

Waziri ataka wadaiwa PPRA kulipa madeni

Na Cynthia Mwilolezi,
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ameziagiza taasisi zote zinazodaiwa gharama za matangazo na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kulipa madeni yao kabla ya Agosti 30, mwaka huu, ili wasichukuliwe hatua.

Akitoa agizo hilo jana katika Kongamano la Saba la Ununuzi wa Umma, lililofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Dk. Kijaji pia aliagiza bodi za taasisi za umma na maofisa masuhuli wote kutoa ushirikiano kwa mamlaka kama ilivyoombwa na Mwenyekiti wa Bodi.

Alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 inaipa PPRA uwezo wa kukusanya mapato, kutokana na huduma za matangazo ya zabuni na pia mafunzo kwa taasisi nunuzi.

"Lakini taarifa ya PPRA inaonyesha kuna changamoto kwenye eneo hili la mapato, ikiwa pamoja na taasisi nunuzi kwa makusudi kuacha kulipa gharama za matangazo mara baada ya mamlaka kutimiza wajibu wake wa kisheria," aliisema.

Dk. Kijaji alisema kuacha au kuchelewesha malipo ya huduma zilizotolewa ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha PPRA kutekeleza majukumu yake ya msingi, ikiwamo kufanya ukaguzi.

Alisema gharama za matangazo wanazotakiwa kulipa PPRA ni ndogo ikilinganishwa na gharama zilizopo katika soko, hususani magazeti.

"Sasa nikiwa waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya ununuzi wa umma, naziagiza taasisi zote zinazodaiwa gharama za matangazo na PPRA, kulipa madeni yao kabla ya Agosti 30, mwaka huu. Asiyelipa hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya maofisa masuhuli watakaokaidi agizo hili," alisisitiza.

Pia alisema pamoja na marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma yaliyofanyika mwaka 2016, bado kuna kelele kutoka kwa wadau kuhusu ugumu wa utekelezaji wa sheria hiyo.

"Je, tatizo ni sheria au uelewa wa watu? Agizo langu kwenu ni kwamba moja ya maazimio ya kongamano hili iwe ni kuainisha mambo yanayolalamikiwa na wadau kwenye ununuzi wa umma. Baada ya marekebisho ya sheria na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kukabiliana na malalamiko hayo, ili kuakisi dhamira njema ya serikali," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Leonard Kapongo, alisema PPRA imezijengea uwezo taasisi nunuzi. Alisema katika kipindi cha serikali hii yaani mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019, maofisa 3,899 wanaohusika kwenye ununuzi wa umma walipewa mafunzo.

Waliopewa mafunzo aliwataja kuwa ni maofisa masuhuli, wajumbe wa bodi za zabuni, watumishi wa vitengo vinavyosimamia ununuzi, wakaguzi wa ndani na watumishi wa idara tumizi.

Alisema PPRA inafanya ukaguzi kila mwaka kutathmini kiwango cha uzingatiaji wa sheria au ukidhi wa matakwa ya sheria kwa ununuzi unaofanywa na taasisi za umma.

Mfanyabiashara wa madini ya Tanzanite, Lomayani Laizer (kulia), akizungumza kwenye harambee ya ujenzi wa kanisa la KKKT Naepo, Kata ya Naisinyai, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Naisinyai, Taikoo Laizer na mfanyabiashara, Mepukori Siria. **PICHA: GIFT THADEY**

Wajasiriamali wa Mirerani wapewa mchongo

Na Cynthia Mwilolezi,
SIMANJIRO

WAJASIRIAMALI 50 wa Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuwa wabunifu kwa kuandaa vitu vitakavyokuwa endelevu kwa jamii na si kupoteza muda kwa kuiga biashara zisizo na tija.

Mtaalamu wa Saikolojia wa jijini Arusha, Joseph Mrindoko, aliyasema hayo jana wakati akiwajengea uwezo wajasiriamali hao kwenye ukumbi wa Mazubu Grand, Mirerani.

Mrindoko alisema wajasiriamali wanapaswa kutambua kuwa wanatakiwa kufanya kazi, kupitia maono ya mioyo yao tangu utotoni kwa kuwa kwa kufanya hivyo, watapata mafanikio.

Alisema kanuni za maisha zinaeleza kuwa "usipofanya chochote hatapata chochote na kadiri unavyofanya ndiyo utakavyopata", hivyo wasibweteke kwenye maisha yao.

"Akili ya binadamu ina sehemu tatu tuzitumie zote na ukiwa duniani hakikisha unaacha alama tusilale mchana. Mfano mimi huu mwaka wangu wa nane nalala kwa muda wa saa nne pekee kwa siku na wala sijaugua ugonjwa wowote," alisema Mrindoko.

Mmoja wa Wakurugenzi wa Asasi ya Tanzanite Mining Tourism, Charles Mnyalu, alisema kupitia mafunzo hayo wajasiriamali hao wataongeza uelewa ili wajinufaishe wao wenyewe na jamii kwa ujumla.

Mnyalu alisema wamedhamini mafunzo hayo kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kuwanyanyua kiuchumi wajasiriamali hao pindi wakizingatia elimu waliyoipata.

Mkurugenzi mwenza wa asasi hiyo, Nuru Mkirery, alisema mafunzo hayo yametolewa bila malipo kwa lengo la kuwajali wajasiriamali hao ili wachangamkie fursa zilizopo.

"Mwalimu Mrindoko amewafundisha wajasiriamali hawa watoke kwenye duara walilopo na kufikiria nje ya hapo kwani binadamu akitumia akili aliyonayo ambayo ni rasilimali aliyonayo anaweza kunufaika maishani mwake," alisema Mkirery.

Mmoja wa wajasiriamali walioshiriki mafunzo hayo, Hamis Seif, alisema, anatengeneza na kuuza mabegi na amefaidika kwa elimu hiyo ikiwamo kuwekeza kwenye muda na kusimamisha jua.

"Katika mafunzo haya, nimejifunza pia umuhimu wa kuwa mtanashati kwani mara nyingi watu wanakihukumu kitabu kutokana na mwonekano wa jalada lake na si kurasa zilizo ndani yake, hivyo tunapaswa kubadilika," alisema.

Mjasiriamali wa mboga, Zainabu Mussa alisema amefaidika na mafunzo hayo kwa kutakiwa kuwajali wateja na kuthamini biashara yake ikiwamo kuiboresha kwa kuwafikishia nyumbani kuliko kuwasubiri gengeni.

Mwanafunzi kidato cha pili atoweka nyumbani

Na Cynthia Mwilolezi,
ARUSHA

MWANAFUNZI wa kidato cha pili, Mariamu Steven (16) wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Kaloleni, iliyoko wilayani Arusha, anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwake Julai 8, mwaka huu.

Akizungumza jana jijini hapa katika ofisi za Nipashe, baba yake mzazi Steven Samweli, mkazi wa Engashelatoni Kata ya Engosengiu, alisema mwanawe alitoweka siku hiyo saa 1:00 asubuhi akiwa amevaa sare za shule.

"Aliniamsha asubuhi tusali ili awahi shule, tukasali. Akaondoka akiwa amevaa sketi ya shule rangi ya 'Dark Bluu' na sweta la rangi hiyo hiyo na akabeba begi lake na kumpitia mtoto wa jirani yangu Mary Frack," alisema.

Alisema kwa kawaida shuleni anatoka saa 10:30 jioni na hufika nyumbani saa 12:00 jioni, lakini siku hiyo muda huo ulifika hakurudi wala rafiki yake aliyeongozana naye hakurudi.

Steven alisema baada ya kuona muda umepita, alianza kuulizia kwa kuwapigia walimu simu ya kiganjani ambao walisema hawajamwona siku hiyo shuleni na ndugu zake wa Arusha walioko maeneo ya mbali nao hawakumwona.

"Niliuliza kesho yake kwa ndugu zangu wa Dar es Salaam na Tanga wakaniambia hawajamwona, nikaenda shuleni kuuliza rafiki zake wa karibu nao, walikana kumwona na hata shuleni hakufika siku hiyo," alisema.

Alisema baada ya kuuliza kwa walimu na wanafunzi wenzake ndugu, jamaa na marafiki bila mafanikio alitoa taarifa kituo Kikuu cha Polisi cha Mjini

Arusha na kufungua jalada namba AR/RB/7307/2019 la kumtorosha mwanafunzi chini ya uangalizi wa mzazi.

Mwandishi wa habari wa kituo cha matangazo Radio Faraja, iliyopo Shinyanga Mjini, Josephine Charles, akitoa zawadi za taulo za kike, sabuni za kufulia na kuogeshea watoto, kwenye wodi ya kinamama katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga juzi, wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

Taarifa DC kuomba rushwa yatua Takukuru

Na Paul William, MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kilimanjaro, imethibitisha kupokea malalamiko ya mfanyabiashara na mmiliki wa hoteli ya kitalii ya Weruweru River Lodge, anayedai kuombwa rushwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya.

Kipande cha mkanda wa video kinachodaiwa kuwa na malalamiko ya mfanyabiashara huyo, Curthbert Swai, kilikuwa kikizunguka kwenye mitandao ya kijamii kwa siku chache zilizopita na kuibua mjadala.

Alipotafutwa jana kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Holle Makungu, alikiri taasisi hiyo kupokea malalamiko hayo kutoka kwa Swai, huku akieleza kuwa wanaendelea kuyafanyia kazi.

"Takukuru tunakiri kupokea malalamiko ya mfanyabiashara Curthbet Swai dhidi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na tumeanza kuyafanyia kazi," alisema Makungu.

Katika kipande hicho cha mkanda huo wa video unaodaiwa kuwa wa Swai anasikika akisema: "Mheshimiwa Sabaya, mwaka jana mwezi wa 11, alinipa saa 48 ya kuhamisha akaunti za Weruweru River Lodge kupeleka Hai. Nilifanya kama anavyotaka lakini mpaka sasa hivi hata sijajua kwa nini. Hiyo ni moja, wakati huo huo akawa anadai hotel levy (kodi ya hoteli) ambapo yeye hajui kwamba ukiwa unalipa VAT (kodi ya ongezeko la thamani) hutakiwi kulipa 'hotel levy'."

Mfanyabiashara huyo anaonekana katika mkanda huo akieleza kuwa unachotakiwa kulipa ni 'service levy' (kodi ya huduma). Mheshimiwa yeye kuelewa hicho kitendo cha namna hiyo kilitokea sisi wiki tatu, nikihudhuria kila siku asubuhi hadi saa nane, bila kujua bila kujali huyu ni mteja wake. "Jamani mimi ni mwezenu naumia, akaniambia bwana nataka Sh. milioni tano, mimi nimetumwa na ninafanya kazi ya serikali. Hapo hapo akaniambia unaamua utaisemaje, aidha utasema kwamba 'Makonda style' au ni rushwa unanipa, nahitaji hiyo hela.

"Mheshimiwa nikampa Sh. milioni mbili, bado akaendelea kuninyanyasa ikabidi nitoke kwa mfanyabiashara mwenzangu (anamtaja jina), aliniambia we mpe tu, na kweli nilimpa na mara ya pili nilimpa milioni mbili na mara ya tatu nikampa milioni mbili.

Ujenzi hospitali wilaya wakamilika 90%

Na Godfrey Mushi, SIHA

UJENZI wa majengo sita ya Hospitali ya Wilaya ya Siha ambao umeigharimu serikali Sh. bilioni 1.5, umekamilika kwa asilimia 90, huku ikielezwa kukamilika kwake kutapunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali za rufani.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Andrew Method, alithibitisha kuwa mradi huo utamalizika hivi karibuni ili kuruhusu kuanza kutumika kutoa huduma kwa wagonjwa wanaofikishwa katika hospitali hiyo. Mradi huo unahusisha majengo mapya ya wodi ya mama na mtoto, jengo la kuhifadhia maiti (mortuary), jengo la mionzi, jengo la utawala, jengo la dawa na jengo la kufulia.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Siha imekamilisha mradi mwingine wa jengo la kutolea huduma ya bima ya afya.

Dk. Method alisema: "Kimsingi majengo hayo yamefikia hatua za mwisho za ukamilishwaji, kabla ya kuanza kutumika kwa ajili ya huduma kwa wananchi.

"Majengo haya ni miongoni mwa mapya sita yanayojengwa katika hospitali yetu ya Wilaya ya Siha kwa fedha za serikali."

Hospitali ya Wilaya ya Siha inahudumia zaidi ya wakazi 116,313 (kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012) kutoka katika vijiji 60 vilivyoko wilayani hapa.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani hapa kutoa ekari 40 za ardhi.

Ufaulu mitihani wanufaisha shule

Na Godfrey Mushi, MOSHI

MFUMO wa serikali wa lipa kwa matokeo (EP4R) umepeleka katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Sh. milioni 121.6, baada ya kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2018.

Ofisa Elimu ya Sekondari wa Halmashauri hiyo, Juma Tukosa, alisema jana kuwa fedha hizo tayari zimeelekezwa katika Shule ya Sekondari Langasani iliyoko Kata ya Arusha Chini, Kijiji cha Mikocheni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Ni kweli kabisa kwamba kiasi hicho cha pesa kimepatikana kupitia mfumo wa serikali wa lipa kwa matokeo (EP4R) kutokana na Halmashauri ya Moshi kufanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2018, kwa kushika nafasi ya 13 kati ya Halmashauri 195 za Tanzania.

"Na tumeamua kuzipeleka Langasani ilipokea kiasi hicho katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka fedha 2018/2019 na kuanza kutekeleza miradi ya ujenzi mara moja kulingana na miongozo ya pesa hizo kutoka serikali kuu," alisema.

Kwa mujibu wa Tukosa, pamoja na changamoto mbalimbali ikiwamo hali ya hewa, halmashauri hiyo imefanikiwa kusimamia mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa mawili, vyoo sita na bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80.

Tukosa alisema malengo ya ujenzi wa mradi huo wa Sekondari ya Langasani ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Ujenzi wa majengo hayo unatekelezwa na serikali kwa kutumia mafundi wa kijamii maarufu kama 'force account' na kwamba kwa sasa majengo yote yako katika hatua za maboma na mengine katika hatua za kuezekwa paa.

Aidha, mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa umetengewa kiasi cha Sh. milioni 40.

Sambamba na hayo, mradi huo wa vyumba vya madarasa utahusisha uwekaji wa madawati 80, ambapo kila darasa litachukua madawati 40.

Ukurasa 16

Wabunifu, wakadiriaji majenzi bado 'jiwe kuu' uchumi lililoachwa

Ukurasa 14

Waziri aja na operesheni inayowapa maisha mapya wachimbaji wadogo

BUFE

Ijumaa Julai 26, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Boeing 737 hatarini kusimamisha uzalishaji

Ukurasa 15

Waziri Bashungwa: Tumejipanga, hapana shaka tutanufaika maonyesho ya SADC

Na Beatrice Moses

MAONYESHO ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC), yanafanyika nchini Tanzania mwaka huu.

Hiyo imetajwa kuwa ni fursa kubwa kwa wadau wa biashara na wamiliki wa viwanda nchini, ambako wamehamasishwa kushiriki, serikali ikiahidi kuendelea kutafuta suluhisho kwa changamoto zinazowakabili.

Waziri wa Viwanda na Biashara Innocent Bashungwa, anasema serikali iliyoko madarakani imejikita katika kuhakikisha inatimiza ahadi ya kufanya Tanzania kuwa ya Viwanda.

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

Habari katika picha

Ukurasa 17

Wafanyabiashara Pwani waondolewa 'ukope' usajili biashara kimtandao

Ukurasa 20

UCHUMI

Waziri Biteko aja na operesheni maisha mapya wachimbaji wad

• Ashtukia 'janja' ukwepaji kodi na utapeli • Ajira mpya mbadal wa mgodi uliofungwa • Halmashauri Kahama yapata pa kuheme

Wachimba madini wakiwa kazini, **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Na Shaban Njia, KAHAMA

WILAYA ya Kahama iko katika maeneo ambayo yanakuwa kwa kasi mkoani Shinyanga, mzizi wa kasi hiyo ikitajwa ni kilimo pamoja na sekta ya madini.

Wananchi wake ambao ndio nguvu kazi ya mageuzi hayo, wanaelezwa kujishughulisha kwa bidii katika uchimbaji mdogo mdogo wa madini ya dhahabu, hazina iliyopo kwa kiwango kikubwa.

Kabla ya kuanza migodi hiyo midogo iliyozagaa katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na ile ambayo ni rasmi huku mingine ikichimbwa na wachimbaji hao ikimilikiwa na leseni za watu wengine.

Awali, Wilaya ya Kahama yenye Halmashauri tatu, ilikuwa ikitegemea mapato yake ya ndani kwa sehemu kubwa kutoka katika migodi miwili, ambayo ni Acacia Buzwagi na Bulyanhulu, kupitia tozo mbalimbali zilizokusanywa.

Baada ya migodi huo kusimamisha uzalishaji kwa kipindi kirefu, sasa halmashauri hizo mapato yake yanaelezwa kupungua kwa kiwango kikubwa, hata halmalshauri kuingia katika mikakati ya kubuni vyanzo vipya vya mapato, ili kuhimili kujiendesha.

Vyanzo hivyo vipya zaidi imejikita kiatika machimbo ya wachimbaji wadogo, ambayo yamekuwa yakifumuka kila siku katika sehemu mbalimbali na kutengeneza ajira kwa vijana wengi waliopo vijijini, vivyo hivyo kwa walioko mijini waliokosa kazi.

> **Waziri wa Madini Dotto Biteko, alifanya ziara katika kijiji cha kakola Kata ya Bulyanhuru katika Halmashauri ya Msalala, kunakofanyika uchimbaji mdogo.**

Mageuzi hayo yanafanya kuibuka viwanda vingi vya uchenjuaji madini ya dhahabu katika maeneo mbalimbali ya Kahama, huku Halmashauri ya Mji wa Kahama, ikiwa na viwanda vya uchenjuaji zaidi ya 17 vinavyoibua ajira mpya kwa vijana wa maeneo hayo.

Machimbo hayo madogo yaliyoibuka yako katika maeneo ya Mwazimba, Mwime Nyangalata, Mwabomba, Kakola Namba Tisa na Namba mbili.

Pamoja na hatua hiyo, kama ulivyo usemi 'kizuri hakikosi kasoro' baadhi ya madalali, wamiliki wa mashine za uchenjuaji na wanunuzi wake, wanadaiwa wamekuwa wakikwepoa kulipa kodi za serikali na wengine wakidiriki kutorosha madini kwenda katika nchi za jirani za Kenya na Uganda.

Hivi karibuni Waziri wa Madini Dotto Biteko, alifanya ziara katika kijiji cha kakola kata ya Bulyanhuru katika Halmashauri ya Msalala, kunakofanyika uchimbaji mdogo.

Katika ziara hiyo alibaini baadhi ya wamiliki wa mashine za uchenjuaji madini ya dhahabu, wanakwepa kulipa mrabaha wa serikali na wengine hawana hata

Naibu Wazir Madini, Stan Nyongo (kul Mkuu wa W ya Kahama, amringi Mac wakiangalia batili ya 'ste iliyotumiwa ziara ya kus katika kamp kuchenjua m iliyoko Kaha Machi mwak

i inayowapa dogo Kahama

la
ea



daftari la kumbukumbu za mauzo yao.

Pia, alibaini baadhi ya mashine za uchenjuaji zimekuwa zikitumia nyenzo za 'steel wire' katika uchenjuaji, hali anayoieleza kiufundi inawaibia wachimbaji wadogo waliopeleka mchanga wao kwa ajili ya kupata huduma.

Waziri Biteko anasema, kutokana na baadhi ya mashine hizo kubainika kutumia ujanja, alizifunga kwa muda kufanya kazi hiyo ya uchenjuaji mpaka watakapojirekebisha katika suala zima la uchenjuaji madini wanayowasilishiwa .

Biteko anasema, kila mchimbaji mdogo anatakiwa kuhakikisha kuwa madini yake anauza katika maeneo au masoko yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya kuuza madini yao na si pengine, ili kuweza kulipa mapato kwa serikali.

Anasema kuwa, wilayani Kahama, tayari kuna eneo maalumu lilolotengwa katika ofisi za zamani za Halmashauri ya Msalala, kwa ajili ya wanunuzi wa dhahabu, sambamba na kuuza madini mengi.

Anaongeza, eneo hilo lipo katika kijiji cha Kakola, Waziri Biteko, anafanya msako wa kuwabaini wanunuzi wa dhahabu wanaokwepa kulipa kodi za serikali kati ya nyumba hadi nyingine na kuweza kuwakamata baadhi ya wafanyabiashara hao, wakifanya kazi za uchenjuaji.

Pia, kuna madai ya kuwapo wanaotumia nyumba za kulala wageni wanaozigeuza kuwa ofisi na uchenjuaji madini na hadi sasa kuna jumla ya wafanyabiashara 12 wanaotajwa kukwepa kodi na kodi wanaotajwa kuzisafirisha kwenda jirani za Kenya na Uganda.

Waziri Biteko anasema, serikali imeamua kuweka utaratibu kwa wamiliki wa mialo katika maeneo yao, kuhakikisha wanakuwa katika eneo moja na sio kuweka kiholela

"Wamiliki wa mialo katika utafutaji wao wa dhahabu kwenye mchanga wamekuwa wakitumia sumu aina ya 'synaid' katika kukamata madini, sasa inapotapakaa kwenye makazi yao inahatarisha maisha ya wananchi na mifugo wao," anasema Biteko.

Waziri anasema, wenye mialo hiyo wamekuwa wakikaa pamoja wanaweza kuunda vikundi vya watu 10 na kuwachagua watakaowaongoza, kufikia hatua ya kujenga urahisi kukopesheka na halmashauri kwa riba nafuu.

OFISA MADINI

Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga, Joseph Kumbulu, anasema ni marufuku madalali na wanunuzi wa madini ya dhahabu na almasi, kufanya biashara zao katika maeneo ambayo sio rasmi, bali waende kwenye masoko yaliyotengwa na serikali.

Anasema, katika Wilaya ya Kahama, tayari kuna ofisi zimeshajengwa na kilichobaki ni Halmashauri ya Mji Kahama, kuingia mikataba na wapangaji wake ambao ni wanunuzi wa madini, kutoka kwa wachimbaji wadogo na madalali wa madini.

Kumbuli, pia anawataka madalali wa madini kutokaa mjini na wanatakiwa kwenda kwenye maeneo ambayo yalitengwa na serikali, kulingana na mauzo ya dhahabu yaliyopo kutoka kwa wachimbaji wadogo.

Pia, anatahadharisha kwamba, Ofisi ya Madini haitawajibika kwa dalali yeyote mwenye leseni ambaye hatakuwapo katika eneo lisilotambulika rasmi, huku akisisitiza utoaji leseni utafanyika kulingana na makubaliano ya pande zote mbili.

Taahadhari iliyopo ni kwa mnunuzi atakayebainika kuuza madini nje ya soko la dhahabu linalotambulika kisheria, atalazimika kulipa faini ya gharama ya mzigo, kulipa kodi ya serikali na mali hiyo inataifishwa.

"Kwa sasa, serikali imesema kwa atakayebainika kuuza madini hayo katika masoko ambayo sio rasmi, atalipa gharama zote na faini za mzigo aliyokamatwa nayo na kutaifishwa mali zake zote atakazokuwa nazo," anasema Kumbulu.

Kumbulu anaongeza:"Nilikuwa niende kakola tangu juzi kwani huko kuna mifuko zaidi ya elfu moja imekamtwa kwa watu wakitaka kuzitorosha na kwa sasa nimeweka ulinzi wa polisi, kuhakikisha kuwa wanailinda mpaka nitakapofika na kujiridhisha uhalali wake."

Ofisa Madini anabainisha maeneo mengine ya ununuzi wa dhahabu, ni Mwakitoliyo katika Halmashauri ya Shinyanga Vijijini na kwamba yalitengwa katika maeneo matatu. Mpaka sasa kuna maeneo mawili yamekwishapatikana yenye wachimbaji almasi.

Kumbulu anaendelea kusema, kutokana na serikali kutenga maeneo hayo, hali imebadilika kibiashara kwa wanunuzi kuanza kuuza dhahabu katika masoko ya serikali, kinyume na zamani walinunua kiholela na kukwepa kodi.

Waziri pia, alishawahi kufanya msako akishirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kahama, pamoja na Ofisa Madini wa Mkoa Shinyanga, waliofanya msako katika kijiji cha Kakola kubaini wanunuzi wa dhahabu wakifanya biashara kwenye masoko batili.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko.

ri wa
nslaus
ia) na
ilaya
An-
cha,
nyenzo
eel wire'
, katika
htukiza
uni ya
nadini
ama,
ka huu.

Boeing 737 hatarini kusimamisha uzalishaji

Ndege aina ya Boeing 737 Max. **PICHA: MTANDAO**

KAMPUNI ya kutegeneza ndege aina ya Boeing, imetangaza kwamba huenda ikafunga kabisa uzalishaji wa toleo la ndege aina ya Boeing 737Max.

Hadi sasa ndege hiyo imezuiwa kutokana kifanya kazi ikidaiwa kuwa na hitilafu kadhaa za kiufundi.

Inasema kuwa, hadi sasa kampuni hiyo yenye makazi yake nchini Marekani katikia kipindi hicho tajwa tangu Machi iliyoipitwa, imeshapata hasara ya Dola za Marekani bilioni 3.4 Pamoja na kauli hiyo iliyoko katika ripoti yake ya robo mwaka, bosi mkuu wa Boeing, Dennis Muilenburg, kwa upande wa pili anaeleza kujiamini kuwa ana imani kubwa ndege hiyo itarejea kazini hadi ifikapo Oktoba ijayo

"Wakati juhudi zetu za kupigania Boeing 737 Max irejee kazini salama, tuatendelea kutathmini mipango yetu ya uzalishaji," anasema Muilenburg.

Ndege hiyo ilisimamishwa, kupisha kufanyiwa uchunguzi wa usalama wake kiufundi kutokana na kusababisha ajali mbaya kwa Shirikia la Ndege Ethiopia na kusababisha vifo vya watu 157.

Miezi mitano kabla, ndege ya aina hiyo yenye wateja katyika nchi 150 duniani, ilichangia vifo vya abiria 189 katika ndege ya shirika lingine tofauti.

Mkuu huyo wa kampuni ya Boeing, anasema timu yake ya watalamu wa kiufundi wamekuwa wakikutana kila wiki kutathmini huku kukiwepo nyenzo mbadala unatiliwa shaka na unafanyiwa majaribio, sasa imeshafanyiwa majaribio kwa safari 225 hadi sasa.

Anasema: "Huu ni wakati wa changamoto. Kwanza, kwa familia na wapendwa waliokumbwa na haya matukio ya karibuni na waliojitolea kufanya kazi bikla ya kuchoka kutusaidia dhamira yetu ya kutuunga, kutulinda, kuchunguza na kuhamasisha dunia kuhusu usalama na mshikamano."

Muilenburg anasema, tangu kutokea ajali, kiasi cha uzalishaji wa ndege zao za Boeing 737 Max kilipungua kutoka ndege 52 kwa mwezi hadi 42. Anasema, mabadiko hayo ya kuingia gharama kubwa iatika uzalishaji unawafanya waingie gharama kubwa, ikiwamo kununua vifaa vipya zaidi, faida kushuka ambayo inaelekea katika kuisimamisha uzalishaji kwa jumla, iwapo mwelekeo wa hasara hiyo utaendelea.

Ni kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.

BIASHARA

DK. BULAMILE;

Wabunifu, wakadiriaji majenzi bado ‘jiwe kuu’ uchumi lililoachwa kando

• Atangaza mkakati bodi yao kuwaibua

Wajumbe wa mkutano wakimsikiliza Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Mashauriano wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi kwa Mwaka 2017, kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Kikwete mkoani Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Na Yasmine Protace

BODI ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kusimamia Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, ikiwajibika chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk.Ludigija Bulamile, anataja dira yao ni kuwa msimamizi mwenye uwezo na maarifa ya ubunifu, ukadiriaji majenzi na utaalamu unaoshabihiana nao.

Anasema, asasi hiyo ina ofisi tano za kanda anazozitaja: Ziwa, Kaskazini, Kati, Nyanda za Juu Kusini na Mashariki, ikifanya kazi ya kusajili na kuwaratibu wabunifu majengo, wakadiliaji majenzi na kampuni zao.

Dk. Bulamile anasema, hadi kufikia Juni 26 mwaka huu, bodi ilishasajili wataalamu 1,596 na kampuni za kitaalamu 373.

“Wakati bodi ilipoanza shughuli zake mwaka 1998 kulikuwa na wataalamu 188 na kampuni 53,” anasema Dk Bulamile, hatua iliyofikiwa sasa ni kubwa zaidi, ingawaje katika uhalisia mahitaji ni makubwa zaidi.

USAJILI WA SASA

Dk. Bulamile anasema, katika kuhamasisha usajili wa wataalamu na kampuni zao, bodi imepunguza muda kutoka miezi mitatu hadi wastani wa wiki mbili, kwa maombi yaliyokamilika.

> **Kwa robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019, bodi imekagua miradi 1213, lengo lipo la kukagua miradi 1725 nchi nzima.**

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan akisalimiana na wajumbe wajumbe wa mkutano baada ya kufungua mkutano huo.

Anasema katika ukaguzi wa miradi ya ujenzi, bodi hiyo inalenga kuwa na wataalamu waliosajiliwa wanaohusishwa katika ubunifu ,ukadiriaji na usimamizi wa kazi.

”Kwa robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019, bodi imekagua miradi 1213, lengo lipo la kukagua miradi 1725 nchi nzima,” anasema Bulamile.

Anafafanua kuwa, waendelezaji wa wataalamu waliobainika kukiuka sheria, walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo; ikijumuisha kutozwa faini, kusimamishwa usajili na kushitakiwa mahakamani.

Dk. Bulamile anasema, katika mwaka fedha 2018/2019 kuna mashitaka manne yaliwasilishwa mahakamani.

MAFUNZO MAALUM

Eneo lingine analolitaja ni kuwapo mafunzo kwa vitendo inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria, wakiwahusisha wahitimu katika fani za ubunifu majengo,ukadiriaji majenzi na wanaoshabihiana.

Anataja asasi au mahali watokako wataalamu haoni vyuo vikuu wanakotakiwa kupata mafunzo kwa vitendo, kwa muda usiopungua miaka miili .

Mwenyekiti huyo anasema, tangu mwaka 2005, bodi ilianzisha mpango wa kuwafadhili wahitimu kupata mafunzo mara baada ya kuhitimu elimu ya juu unaojulikana kwa jina ‘Enhanced Articled Pupilage Programme’ ambao ni ya mwaka wa pili.

Dk. Bulamile anasema, hadi kufikia Desemba mwaka jana, kuna jumla ya wahitimu 280 walionufaika na mpango huo, wastani wa asilimia 80 wameshasajiliwa na bodi.

Anaongeza kuwa, semina za mafunzo endelevu zinalenga kuwapatia ujuzi mpya unaotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

Bosi na mataalamu huyo, anasema tangu mwaka 2003 hadi sasa, kuna jumla ya wataalamu 6,644 walionufaika na mafunzo hayo na baada ya kila nusu mwaka ,bodi imeendesha walau semina moja.

Pia, anasema kuna mihadhara ya kitaaluma, ambayo bodi imekuwa ikiandaa mihadhara kwa wataalamu wake tamngu mwaka 2005 na wadau wa sekta ya ujenzi ambako kuna jumla ya miadhara 29 iliyofanyika kuwanufaisha wadau 3,200 katika sekta ya ujenzi.

USAJILI

Dk. Bulamile anaeleza kuhusu kusajiliwa miradi ya ujenzi, wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi, kwamba wanatakiwa kusajiliwa miradi yao kabla haijaanza, lengo ni kuiwezesha bodi kufuatilia na kuidhibiti iwe na ufanisi.

Mtaalamu huyo anaeleza kuwa hiyo ni fursa kwa wadau wa sekta ya ujenzi, ikiwamo serikali kupata takwimu za miradi inayoendelezwa kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili mwaka huu, bodi imesajili miradi ya ujenzi 633, huku dira yake kuu ni kusajili miradi 690. Kwa maana hiyo imebaki 63 kufikia lengo lililopangwa.

CHANGAMOTO

Dk. Bulamile anataja kuwa taaluma yao bado haijafahamika vyema katika jamii, hali inayowafanya waendelezaji miradi ya majengo kutowatumia na miradi inaishia kutokuwa na viwango vyenye thamani.

Anasistiza kuwa wataalamu hao ni muhimu katika maendeleo ya taifa, masikitiko yake ni kwamba, licha ya idadi ndogo kulinganisha na mahitaji, hawapatiwi nafasi ya kuajiriwa katika maeneo yenye miradi ya miundombinu na majengo, hasa katika halmashauri mbalimbali nchini.

Dk. Bulamile, anaeleza hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo ni kuwaelimisha wananchi na taasisi kuhusu majukumu yake na umuhimu wa kuwatumia katika shughuli za ujenzi .

DIRA YAKE

Mtaalamu huyo anasema, bodi imezindua mkakati mpya wa mawasiliano, unaoainisha mbinu mpya na za kisasa kujitangaza kwa jamii na inaendelea kufuatilia, ili serikali ikamilishe mchakato wa kutambua taaluma zao katika mfumo wake wa utumishi, kwa manufaa ya umma.

Katika hilo, bodi anasema bodi inaendelea kuzihamasisha vyuo vikuu vya serikali na binafsi, kuanzisha vitivo vyenye fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi .

“Tunafurahi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kimeanzisha mafunzo katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Hiki kitakuwa chuo kikuu cha tatu kutoa mafunzo katika taaluma hizi,” anasema.

Dk. Bulamile anavitaja vingine ni Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya.

MTAALAMU WA BODI

Mtaalamu, Mbaraka Igangula, kutoka bodi hiyo anasema kwa kiasi kikubwa nyumba zilizojengwa nchini, haziko kwenye mpangilio sahihi, kutokana na kukosekana wataalamu sahihi wa ubunifu majenzi na ukadiriaji majenzi.

Anashauri kwamba, jamii inapaswa kuwashirikisha wataalamu wa majengo namna ya kujenga katika maeneo yanayofaa na kuwaelewesha wasijenge katika maeneo yasiyofaa.

“Tunaona hata mvua zinaponyesha, madhara makubwa yanatokea maji kujaa, mawasiliano kukosekana na kwenda maeneo mengine kutokana na maji kujaa.

‘Hiyo inatokana na ujenzi holela ambao haukufuata taratibu za wataalamu wa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi,” anasema Igangula.

Anaiasa jamii kuwafuata wataalamu wanaobuni ramani za ujenzi, huku akiwashutumu wanaouza ramani za nyumba kiholela, akitaja kuwa ni chanzo cha nyumba kujengwa chini ya kiwango, ikibeba makosa ya kiufundi.

Anasema mtu anayejenga nyumba kwa kufuata taratibu kutoka kwa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi, daima nyumba yake inajengwa kwa gharama nafuu.

MAJI JANGWANI

Igangula anazungumzia mafuriko ya maji eneo la Jangwani, jijini Dar es Salama, ambako kujaa maji kunatokana na kutokuwapo mitaro ya kupitisha maji.

“Mvua inaponyesha maji yanatoka mto msimbazi yanakuja jangwani hayana sehemu ya kutokea, hivyo inatakiwa kuchimbwa mitaro ambayo itasaidia kuyasafirisha maji kuelekea baharini,” anasema.

Biashara katika picha

Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya UBA Tanzania, Usman Imam Isiaka, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu kuwaunganisha wajasiriamali katika Jukwaa la Biashara la UBA Marketplace litakalowawezesha kutangaza na kuuza bidhaa zao kupitia mtandao.Kushoto ni Ofisa Uhusiano na Habari wa benki hiyo, Anitha Palangyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Michezo ya kubahatisha ya Biko, Charles Mgeta, kulia akizungumza jambo katika uzinduzi wa kibiashara kati ya Biko na Kampuni ya Vodacom kupitia bidhaa ya Mpesa, ambapo wachezaji wa Biko wanaotumia mpesa watakuwa na droo yao mbali na droo za kawaida za Jumapili na Jumatano. Wengine pichani ni Arjuun Dhillon, ambaye ni Mkurugenzi Kitengo cha Biashara kutoka Vodacom na Ali Z Ali Mkuu wa Kitengo Cha uzalishaji cha wateja wakubwa wa Vodacom. **NA MPIGAPICHA WETU**

Mchuuzi wa matunda aina ya fenesi, akiyaandaa wakati akisubiri wateja katika Mtaa wa Libya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

BIASHARA

WAZIRI BASHUNGWA:

Tumejipanga, hapana shaka tutanufaika maonyesho SADC

Rais Dk. John Magufuli, akikata utepe mara baada ya kuweka jiwe la msingi la kiwanda cha kutengeneza vigae, Mkuranga, Pwani.

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Innocent Bashungwa, akizungumza kwenye moja ya mikutano na maofisa wa wizara yake.

INATOKA UK.13

Anasema katika kufanikisha hilo, wamejipanga kuhakikisha sheria na sera zinazokwaza biashara na uendeshaji wa viwanda nchini zinapitiwa upya ili kufanyiwa marekebisho yatakayosaidia kujenga mazingira rafiki.

Bashungwa anasema, marekebisho hayo yatasaidia pia kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini.

Anasema, hatua hiyo itawezesha ushiriki mzuri katika ushindani wa bidhaa kwenye masoko mbalimbali ya kimataifa, ikiwamo kwenye nchi wanachama wa SADC.

> **"Maonyesho yatafanyika katika Kituo cha JNICC jijini Dar es Salaam, tarehe 5 - 9 Agosti 2019.**

Kwa mujibu wa Bashungwa, hatua hiyo itasaidia kufanikisha maono ya Rais John Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Mapema wiki hii, Waziri Bashungwa alizungumza na waandishi wa habari mapema, kufafanua kuhusu maadhimisho na maonyesho yajayo ya awamu ya nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Bashungwa anaeleza kuwa hiyo ni fursa kubwa kwa Tanzania na Watanzania, wanaopaswa kutumiwa vyema na wadau, kwa kuwa maadhimisho na maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya SADC ni hatua mojawapo ya kuonyesha kwa vitendo utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa SADC (2015- 2063).

Anasema, serikali kupitia wizara yake wanafanya juhudi za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa ujumla, hivyo wanapitia sheria na sera zinazohusiana na masuala ya biashara ili zile zenye vikwazo zitapelekwa bungeni Septemba, ili kufanyiwa marekebisho.

Anataja baadhi ya sera zinazotarajiwa kupitiwa upya ni pamoja na Sera ya Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo na waKati (SMEs) ya mwaka 2003 ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Sera Endelevu ya Maendeleo ya viwanda ya mwaka 1996 ambayo mwisho wake ni 2020 na inayohusu mazao ya kilimo.

Maonyesho hayo yatafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, tarehe 5 - 9 Agosti 2019.

Maadhimisho hayo yatafunguliwa rasmi tarehe 05 Agosti 2019 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli ndiye atakuwa mgeni rasmi katika maonyesho hayo.

Aidha, yanarajiwa kufungwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Ali Mohamed Shein Agosti 8 Mwaka huu.

Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ni Mazingira Wezeshi ya Biashara kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu ya Viwanda.

Maonesho yatawakutanisha wazalishaji na wadau mbalimbali wa bidhaa za viwandani na wafanyabiashara kutoka nchi 16 za SADC.

"Kupitia Maonesho hayo, washiriki watapata nafasi ya kufanya majadiliano ya kibiashara na kutangaza bidhaa hususan zile zinazotengenezwa katika nchi za SADC.

MKAKATI 2015- 2063

Hatua hiyo ni ya mkakati unaolenga kuongeza kasi ya kuimarisha ushirikiano na ushindani wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa SADC.

Mkakati huo umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni uendelezaji viwanda (industrialization); Ushindaji (competitiveness); na Mtangamano wa Kikanda (regional integration).

Utekelezaji wa Mkakati huo unaenda sambamba na utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya SADC (1996).

Wizara ya Viwanda inabainisha kuwa kupitia juhudi hizo Tanzania imekuwa inafanya vizuri katika ufanyaji wa biashara katika Jumuiya ya SADC.

Mauzo ya Tanzania kwenda nchi za SADC kwa mwaka 2018 yalikuwa Dola za Kimarekani Milioni 999.34 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani Milioni 877.8 mwaka 2017.

Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.16%. Wakati huo uingizaji wa bidhaa Tanzania kutoka SADC uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 600.64 mil mwaka 2017 hadi kufikia Dola za Kimarekani 604.32 mil mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 0.61.

Baadhi ya bidhaa muhimu ambazo Tanzania inauza SADC ni pamoja na madini mbalimbali kama vile Tanzanite na Dhahabu; bidhaa za kilimo kama vile Chai na Kahawa.

Nyingine ni bidhaa za viwandani kama vile plastiki, sigara, saruji, marumaru, na madawa na vifaa tiba.

Bidhaa ambazo Tanzania inanunua kwa wingi kutoka nchi za SADC zinahusisha magari, mbegu za mahindi, gesi, mabati, vilainishi (lubricants) na sukari. Bidhaa hizo zaidi zinatoka katika nchi za Afrika Kusini, Zambia, Mauritius na Malawi.

Vilevile, Tanzania inanufaika na miradi mbalimbali ya ushirikiano inayotekelezwa katika nchi za SADC, hususan miradi inayounganisha nchi jirani.

Miradi hii ni kama vile mradi wa maendeleo ya nishati ya umeme unaounganisha Tanzania na Zambia, mradi wa vituo vya pamoja vya forodha vya mpakani (OSBP), kati ya Tanzania na Zambia (Tunduma).

BIASHARA

Tumejipanga, hapana shaka tutanufaika maonyesho SADC

MIRADI MIKUBWA

Mradi wa Maendeleo ya Maji na uendelezaji wa Bonde la mto Songwe Tanzania na Malawi (Nakonde), Mradi wa Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, uimarishaji miundombinu ya reli ya Tazara na bandari.

Hivi sasa Tanzania inatarajia kuwa mzalishaji, mfanyabiashara na mwananchi kwa ujumla, watapata fursa mbalimbali zitakazotokana na Maadhimisho na Maonyesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda na Tanzania, kuwa Mwenyekiti wa SADC.

Waziri Bashungwa anawahamasisha wadau na wananchi wote kuchangamkia fursa hizo, ambazo anazinashiri zitaongeza chachu ya kufanya vizuri zaidi katika uendelezaji viwanda nchini.

Hadi tarehe 22 Julai 2019, jumla ya washiriki waliojiandikisha imefikia 531, katoi yao 345 ni Watanzania.

Pia, inaelezwa washiriki hao 531 waliojiandikisha, waonyeshaji walioko idadi yao iko 204, kati yao 158 ni Watanzania.

Kwa mantiki hiyo, washiriki 327 watakuwa wamejisajili kwa ajili ya kushiriki mijadala mbalimbali na kutembelea maonesho.

"Hii inadhihirisha kuwa juhudi zenu za zinaleta manufaa kwa kuwa Watanzania wengi wamehamasika kushiriki. Tunawaomba mzidishe juhudi zenu ili kufikia lengo la serikali la kuwa na washiriki kati ya 800 hadi 1000," anasema Bashungwa.

Taasisi ya Sekta binafsi Tanzania (TPSF) imeipongeza Serikali ya awamu inayoongozwa na Rais Magufuli kwa kuonyesha nia madhubuti ya kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

MKUU TPSF

Katibu Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, anasema kuwa kuna ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuimarika kwa majadiliano kati yao na serikali.

Pia, anaeleza faraja yake kwa sekta binafsi kushirikishwa katika hatua mbalimbali za maandalizi, pia kupatiwa nyenzo muhimu na serikali zinazowawezesha kuwa washiriki wenye viwago vya kimataifa.

"TPSF imeshuhudia utayari na mwitikio mkubwa kwa upande wa serikali kukutana na kujadiliana na sekta binafsi katika ngazi zote za wilaya, mikoa na taifa na tayari mafanikio yameanza kuonekana," anasema Simbeye.

Pia, anafafanua kuwa:"Mojawapo ya mafanikio ambayo TPSF inajivunia ni kuimarika kwa majadiliano yenye tija kati ya sekta ya umma na sekta binafsi."

Anasema, kuna mawaziri wapatao saba kwenye mikoa mbalimbali, pamoja na mambo mengine walitumia muda huo kuzungumza na wadau wa sekta binafsi.

Katibu Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, akiwa katika moja ya mikutano na wafanyabiashara, jijini Dar es Salaam.

> **"Hii inadhihirisha kuwa juhudi zenu za zinaleta manufaa kwa kuwa Watanzania wengi wamehamasika kushiriki. Tunawaomba mzidishe juhudi zenu ili kufikia lengo la serikali la kuwa na washiriki kati ya 800 hadi 1000.**

Wafanyabiashara wajumbe wa TPSF, ambao ni washiriki wa maonyesho hayo, wakiwa katika moja ya mikutano inayowahusu. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**

Simbeye anatumia nafasi hiyo kuwakumbusha wafanyabiashara kutochanganya siasa na biashara, akibainisha taasisi hiyo ikibaini itawafuta uanachama.

Anasema pia TPSF imekusudia kujadili mambo mbalimbali na wadau wake, ikiwamo jinsi wanavyoweza kupandisha kiwango inachochangia sekta binafsi kwenye pato la taifa, kutoka asilimia 12 za sasa, hadi asilimia 15 au zaidi.

Katibu Mtendaji huyo anabainisha kuwa, wanatamani wadau wa sekta hiyo waitumie mikutano hiyo pia kutoa mawazo ya mwongozo wa kuboresha sheria za udhibiti nchini.

Anasema, licha ya serikali kuwa na mipango mizuri ya kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini, kumekuwapo tatizo la kuchelewesha utekelezaji wake, hivyo inakuwa kikwazo cha kusonga mbele katika kasi ya maendeleo kitaifa.

Simbeye anatoa mfano wa bandarini, ambako pametajwa na wadau kuwa ni kiwazo kwa kuwa na utaratibu mrefu wa utoaji wa mizigo, lakini bado haijashughulikiwa.

UCHUMI

Wafanyabiashara waondolewa 'ukope' usajili biashara kimtandao

• Waanikiwa urahisi, vigingi vya kutosajili

Na Yasmine Protace, Mkuranga

MFUMO wa kusajili biashara kwa njia ya mtandao, unaelezwa kuwa muhimu na utakaowarahisishia wafanyabiashara kujisajili wakiwa katika maeneo wanayoishi.

Kuanzishwa kwa mfumo huo pia kutawaondolea wafanyabiashara usumbufu wa kuzifuata ofisi za makao makuu Jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kufanya usajili.

Mkurugenzi wa Utawala na Fedha kutoka Wakala wa Taifa wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), Bakari Mketo, anasema pia ni mfumo utakaowezesha na utasaidia kuzibaini kampuni hewa.

Alitoa ufafanuzi huo kwenye mafunzo ya siku nne yaliyofanyika katika wilaya ya Mkuranga na Kibaha mkoani Pwani.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Brela yenye lengo ni kutoa elimu kuhusu usajili kwa njia ya mtandao, yaliwashirikisha wafanyabiashara na maofisa biashara wa wilaya hizo .

Mketo anasema, lengo la kuanzishwa kwa mfumo huo wa kusajili biashara kwa njia ya mtandao, ni kumrahisishia mfanyabiashara katika usajili.

"Zamani ilikuwa wanatumia 'kabrasha' kwenda makao makuu kwa ajili ya kusajili biashara zao," anasema Mketo. Anaongeza kuwa mfumo huo wa kisasa, utasaidia kuondoa urasimu kwa wateja na watakuwa wanazungumza na mfumo na sio mtu mwingine au wa kati.

Anaongeza kuwa leseni za biashara zinalipiwa kuendana na biashara itakayokuwa inaifanyika na katika usajili, ni lazima mtu kuwa na kitambulisho cha taifa kutimiza matakwa.

Kwa mujibu wa Mketo kampuni zilizosajiliwa kupitia mfumo huo tangu mwezi Februari mwaka huu hadi sasa jumla ni 16,205.

" Kampuni zilizosajiliwa alama za biashara kupitia mfumo ni 64,700 na leseni za viwanda 7,130 mpaka sasa zilisajiliwa kwa mfumo," anasema.

Mketo anafanya kwamba, kwa waliofungua kampuni na kushindwa kuziendeleza hawatakiwi kuzifunga, wanatakiwa waendelee kuzilipia kwa kuwa inapotangazwa tenda wanaweza kuingia katika ushindani na wakapewa tenda.

CHANGAMOTO ZIKOJE?

Mketo anasema kwamba, suala la elimu katika matumizi ya mfumo huo kwa baadhi ya wafanyabiashara, umetawaliwa na woga unaohitaji kumalizwa kwa kupatiwa.

Kuna malalamiko kwamba, kuna wakati inatokea changamoto mtandao unatoweka kwa siku kadhaa, hali inayowapa shida wateja husika.

WANUFAIKA WAKE

Judicare Ndegelo Ndosi, ni mfanyabiashara na mfugaji wa kuku na samaki, ni miongoni mwa wafanyabiashara walioshiriki mafunzo hayo, anayekiri kuwa ni mazuri ya yenye manufaa kwao, kwani yatawasaidia katika malipo, ikiwa na matokeo chanya ya kuongeza kipato.

Anasema mfumo huo, utakuwa msaada wa kuwabaini wasio waaminifu katika kuingilia biashara zisizowahusu.

Elina Mgonja, ni Katibu wa Wanawake Jukwaa la Uchumi Mkoa wa Pwani, anasema kuwa elimu iliyotolewa ni ya msingi kwao na inaonyesha nguzo muhimu ya kuwa mfanyabiashara kupitia sharti la usajilii.

Anaongeza kuwa usajili wa biashara unakusaidia kujitangaza na kumuwezesha mtu kunufaika na biashara yake na inazuia mtu asiyesajiliwa kupata mkopo

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Mkoa wa Pwani, Abdallah Ndauka, anasema kuwa elimu wanayopewa itawasaidia kujua sheria na taratibu za kusajili na kukuza biashara zao.

Kwa mujibu wa Ndauka, ni mfumo unaokomesha matapeli ambao hawatakuwa na nafasi ya kuwarubuni wafanyabiashara..

WIZARA MAMA

Liliani Godwini kutoka, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, anasema wizara hiyo ipo bega kwa bega na wafanyabiashara katika kuwaongezea uwezo katika mbinu na nyenzo za kibiashara.

MTAALAMU MFUMO

Francis Mwakalebela, ni mtaalamu wa mfumo kutoka Brela, anayesema kuwa mfumo huo ni rafiki na utawasaidia Watanzania katika uboreshaji wa biashara zao.

Anaongeza kuwa mfumo huo, unaweza kuleta matatizo iwapo itatokea mteja hajatekeleza maelekezo yaliyotakiwa.

Anasema usajili huo wa kimfumo utazisaidia kampuni zote na majina ya biashara yaliyosajiliwa kwa mfumo wa kuandikwa kwa karatasi yanasajiliwa kwa njia ya mtandao.

"Usajili wa biashara ni Sh. 20,000. Kila jina la biashara; ada Sh. 5,000 kwa ajili ya biashara," anasema.

Mwakalebela anaongeza kuwa kusajili kunasaidia kujua biashara anayoifanya mtu na wamiliki wake na kwa ambaye hajasajili, anakosa fursa ya kupata tenda na fursa zingine za kibiashara.

Katika hilo, Mwakalebela anasisitiza kwamba si sahihi kutumia jina la mtu kufanyia biashara na kwa asiye Mtanzania, hatakiwa kumiliki jina la biashara, bali anatakiwa kufungua kampuni.

Washiriki wa mafunzo ya usajili wa kampuni kwa mtandao wa Mkoa wa Pwani, wakiwa katika darasa la mafunzo kwa vitendo la namna ya kusajili kampuni kwa njia ya mtandao. **PICHA ZOTE: BLOGU YA MICHUZI.**

> **"Kampuni zilizosajiliwa alama za biashara kupitia mfumo ni 64,700 na leseni za viwanda 7,130 mpaka sasa zilisajiliwa kwa mfumo.**

Mtaalamu wa Mfumo wa Usajili wa Brela Kanda ya Kusini, Francis Mwakalebela, akitoa elimu ya vitendo kwa washiriki wa mafunzo kuhusu namna ya kusajili kampuni kwa njia ya mtandao.

Kinamama wakiweka kwenye chupa pombe ya kienyeji aina ya wanzuki katika Kitongoji cha Udindivu, wilayani Bagamayo, Mkoa wa Pwani jana. Chupa moja ya wanzuki, huuzwa kwa bei ya 200/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Waingia mitaani kusaka wadaiwa sugu

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAFANYAKAZI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mbeya (Mbeya-WSSA) wameingia mitaani katika maeneo mbalimbali kuwasaka wadaiwa sugu wa ankara za maji na kukata huduma hiyo kwa wateja wasiotaka kulipa.

Wafanyakazi hao wakiongozana na Mkurugenzi Mtendaji mpya wa mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, waliendesha operesheni hiyo juzi. Zaidi ya wateja 20 walisitishiwa huduma akiwamo mfanyabiashara mmoja ambaye alikuwa anadaiwa Sh. 700,000.

Baada ya operesheni hiyo, Mengo alisema mamlaka hiyo inawadai wateja wake zaidi ya Sh. bilioni saba na kwamba lengo la operesheni hiyo ni kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa ajili ya kuboresha huduma.

Alisema kwa sasa kwa mujibu wa sheria za uendeshaji, mamlaka za maji zinatakiwa kujiendesha kibiashara na kwamba wataendelea kuendesha operesheni hiyo kwa kutembea nyumba kwa nyumba ili kuwaelimisha wateja kulipa ankara zao kwa wakati.

"Ili kuiendesha mamlaka yetu kwa faida na kuwahudumia wananchi kwa huduma ambazo ni endelevu, lazima wateja wetu walipe madeni yao. Sasa tumeamua kuingia mitaani ili kuhakikisha tunatimiza azma yetu ya kujiendesha kwa faida," alisema.

Aidha, alisema kati ya Sh. bilioni saba wanazowadai wateja wao, zaidi ya Sh. bilioni moja wanazidai taasisi za serikali zikiwamo Magereza na Polisi.

Mengo alisema kwa sasa ili kupambana na changamoto ya wateja kutolipa ankra zao kwa wakati, wameanzisha mfumo wa kulipia huduma kabla ya kutumia ambao utawafanya wateja wapate huduma baada ya kulipa.

Aidha, alisema mamlaka hiyo itawachukulia hatua kali watumishi wake ambao kwa makusudi wanasababisha wateja wenye madeni makubwa kuendelea kupata huduma kabla hawajalipia kwa madai kuwa kati ya wateja wote waliositishiwa huduma kwenye zoezi hilo, mwenye deni dogo ilikuwa Sh. 80,000.

Baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo ambao wanatekeleza majukumu ya kusoma dira za maji, walisema operesheni hiyo inawasaidia kuboresha uhusiano kati yao na wateja kwa madai kuwa walikuwa wanapatiwa na elimu. Mmoja wa watumishji hao, Jacob Lumambo, alisema kabla ya operesheni hiyo, walikuwa wanakumbana na changamoto nyingi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao hali iliyokuwa inasababisha ufanisi wa kazi kuwa mdogo.

Alisema moja ya changamoto kubwa ni baadhi ya wateja kufungia milango ili kuzuia kusoma dira pamoja na baadhi kuwafungulia mbwa na kuwafukuza.

"Tulikuwa tunafanya kazi katika mazingira magumu sana. Baadhi ya wateja walikuwa hawaitumii elimu tuliyokuwa tunaitoa. Unakuja unatoa elimu lakini ukija siku nyingine unakuta mambo ni yale yale, ukifunguliwa mbwa na mteja lazima ukimbie kujiokoa," alisema Lumambo.

Baadhi ya wananchi waliositishiwa huduma hiyo walidai kuwa awali walikuwa hawaoni umuhimu wa kulipa ankra kwa sababu maji yalikuwa yanatoka kwa shida na hivyo walikuwa hawafurahishwi na huduma.

Mmoja wa wananchi hao, Moses Mwakinafu, alisema kwa sasa wanapata huduma vizuri na kutokana na elimu waliyopatiwa watahakikisha wanalipa ankra zao bila kinyongo na bila usumbufu kwa sababu wanapata maji wakati wote.

Barabara yajengwa kuboresha utalii

Na Nebart Msokwa, MBARALI

SERIKALI imeanza kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mpanga – Kipengele, iliyoko kati ya mikoa ya Mbeya na Njombe ili kuunganisha vivutio vilivyomo na kuwezesha watalii kuvifikia kiurahisi.

Hifadhi hiyo ni miongoni mwa maeneo nchini ambayo yana vivutio vingi vya watalii lakini baadhi yake vilikuwa havifikiki kwa usafiri wa magari kutokana na kutokuwapo kwa barabara, hivyo kutokuwa na faida kwa taifa.

Ofisa Utalii wa Hifadhi hiyo, Emmanuel Silayo, alisema barabara hiyo inajengwa na serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa) ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia hifadhi hiyo na raslimali zilizomo.

Alisema barabara hizo zitatumika pia kuwahudumia wananchi wanaopatikana katika maeneo yote kuzunguka hifadhi ili kuboresha uhusiano na kuwafanya wawe sehemu ya walinzi wa raslimali zinazopatikana.

"Kwa hii awamu ya kwanza tutachonga barabara hii mpaka kwenye maporomoko ya Kimani ambayo yanavutia sana na awamu ya pili tutafika mpaka katika maporomoko ya Makunohila na baada ya hapo tutaanza kuunganisha na vivutio vingine," alisema Silayo.

Alisisitiza kuwa ndani ya hifadhi hiyo kuna vivutio vingi yakiwamo mapango, maua mazuri ambayo yanapatikana katika uwanda wa juu wa safu za milima kipengele na baadhi ya wanyama wakiwamo fisi maji na tandala ambao wanapatikana uwanda wa chini wa hifadhi.

Vilevile alisema wako wanyama wengine wakiwamo ngedere, ndege wanaohamahama kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika na baadhi ya ndege wadogo wakiwamo fundi chuma na ndege mla nyuki (bee eater).

Baadhi ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo, walisema hatua ya serikali kuanza kutengeneza barabara hizo ni habari njema kwao kwa madai kuwa watalii wataongezeka na wao watakuwa wananufaika nao.

Mmoja wa wananchi hao, Elisha Shomile, alisema endapo watalii wataongezeka kwenye hifadhi hiyo, watanufaika kwa kuwauzia bidhaa mbalimbali wanazozalisha kwenye maeneo yao pamoja na kupata vibarua vya kuwatembeza.

"Sisi tunanufaika vizuri sana na hifadhi hii maana maji yote tunayotumia hapa kijijini kwetu yanatoka ndani ya hifadhi lakini kutokana na miundombinu kuwa mibovu huwa tunashindwa kutumia hata baiskeli kwenda kusafisha tangi sasa barabara ikitengenezwa itakuwa rahisi sisi kufika," alisema Shomile.

Pia alisema hata huduma za kijamii ambazo hifadhi hiyo inawapatia wananchi hao itaongezeka kutokana na sekta ya utalii kuwa miongoni mwa sekta zinazoingiza fedha nyingi za kigeni.

Polisi Mbeya waonya madereva wa bajaji

Na Nebart Msokwa, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewawashia moto madereva wanaoendesha pikipiki za magurudumu matatu maarufu kama 'Bajaj' wanaoendesha vyombo hivyo bila kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa kuwakamata na kuwachukulia hatua.

Moja ya makundi yanayolengwa kwenye kamata kamata hiyo ni wale wanaoendesha bajaji hizo bila kuwa na leseni na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ulrich Matei, alisema jana kuwa lengo lao ni kupunguza ajali za barabarani.

Alisema jeshi hilo limebaini kuwa madereva wengi wa vyombo hivyo wanaosababisha ajali wanakuwa hawana leseni wala vyeti vya udereva na badala yao wanakuwa wamejifunza mitaani.

Matei alisema baadhi ya madereva hao wanaendesha vyombo hivyo bila tahadhari na wakiona askari wanajishuku na kuanza kukimbia hali ambayo alisema ni hatari kwa usalama wao na watumiaji wengine wa barabara.

"Ukitaka kufuatilia unakuta wengine eneo la Mafiati imewaka taa nyekundu ambayo haimruhusu kupita yeye anapita. Sasa wengi unakuta hata darasa la saba hakumaliza lakini ameshika chombo cha moto anaendesha kwa hiyo huyo ni rahisi kusababisha ajali," alisema Matei.

Baadhi ya waendesha bajaji jijini Mbeya walisema msako huo ni mzuri na una tija kwao kwa madai kuwa kwa sasa madereva wote wa bajaji wanaonekana wa ovyo kutokana na kasoro za wachache wasiokuwa na leseni.

Mmoja wa madereva hao, Shaibu Juma, alisema dereva wa bajaji ni kama dereva anayeendesha gari. hivyo kuendesha chombo hicho bila kuwa na leseni ni kuhatarisha maisha yake, ya abiria pamoja na watu wengine.

Alisema hatua hiyo itasaidia kila anayetaka kuendesha chombo hicho kuhakikisha anaenda kwanza darasani na kupata leseni itakayomwezesha kuendesha chombo hicho kwa ufanisi.

"Sisi tunawashauri hata matajiri wanaonunua bajaji wahakikishe wanamkabidhi dereva ambaye ana leseni ili kutuondolea hili tatizo la kuchukuliwa kama kundi haramu wakati wengine tuko vizuri na leseni zetu," alisema Shaibu.



Wanafunzi 4,500 wafunzwa usalama

Na Augusta Njoji, DODOMA

KATIKA jitihada za kupunguza ajali barabarani kwenye Jiji la Dodoma ambalo linakua kwa kasi, wadau mbalimbali zikiwamo kampuni ya nishati wametoa mafunzo kwa wanafunzi wa shule za msingi takribani 4,500.

Wadau hao ambao ni pamoja na kampuni ya Puma Energy Tanzania, imetoa mafunzo ya usalama barabarani kwa wanafunzi zaidi ya 4,500 wa shule za msingi kuwafungua macho kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya barabara.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Dominic Dhanah, alisema jana katika tukio la utoaji wa zawadi kwa wanafunzi walioshinda shindano la michoro ya usalama barabarani mwaka huu lililofanyika Shule ya Msingi Kaloleni, jijini Dodoma.

Alisema Puma Energy imeamua kufanya programu hiyo kwa sababu ya ukuaji wa haraka wa jiji ambao shughuli za kijamii na ongezeko la watu na magari vinahatarisha usalama wa watoto wanapokuwa barabarani ikiwa ni pamoja na kwenda shule na kurudi nyumbani.

"Mpaka sasa tumefundisha jumla wanafunzi takribani 4,500 wa shule za msingi katika shule tano za Jiji la Dodoma na tunatoa zawadi kwa wanafunzi wa shule za msingi walioshinda shindano la michoro ya usalama barabarani na tukio hili linahitimisha programu ya mwezi mmoja iliyofanywa na kampuni ya Puma kwa ushirikiano na Shirika lisilo la kiserikali la AMEND," alisema Dhanah. Dhanah alisema programu hiyo pia ilihusisha walimu 15 na ni mwendelezo wa kampeni ambayo ilizinduliwa rasmi mwaka 2013.

"Zaidi ya shule 80 zimefikiwa na jumla ya wanafunzi 100,000 wamepata mafunzo katika mikoa ya Dar-es-Salaam, Geita, Ruvuma na Dodoma, pia maofisa mbalimbali wa polisi hususani kikosi cha usalama barabarani na viongozi wengine wa serikali," alisema.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwapa uelewa watoto hususani wa shule za msingi juu ya namna bora ya matumizi ya barabara kwa kuwa uelewa wao kwenye eneo hilo ni mdogo.

"Tunaamini kwa kufanya hivyo tunawaongezea uelewa kuhusu dhana nzima ya usalama barabarani kwa Watanzania wengi zaidi, zoezi hili pia kwa mwaka huu linafanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na visiwani Zanzibar ambapo shule 25 zitafikiwa," alisema Dhanah.

Aliahidi kuwa kampuni hiyo itaendelea kuongeza wigo ili kufikia shule nyingi zaidi nchini na itaendelea kuwekeza katika kampeni ya usalama barabarani ikishirikiana na serikali kupitia Jeshi la Polisi ili kuokoa maisha ya Watanzania.

Tacaids yataja vipaumbele kupunguza maambukizo

Na Augusta Njoji, DODOMA

TUME ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids) imetaja maeneo manne muhimu yanayopaswa kutiliwa mkazo ili kupunguza maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) ifikapo mwaka 2030.

Maeneo hayo yanayopaswa kuwekezwa na kutilia mkazo ni pamoja na matumizi ya mipira ya kike na kiume -kondomu, tohara kwa wanaume, kudhibiti biashara ya ngono kwa wanawake na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU za ARVs.

Hayo yalielezwa jana jijini Dodoma na Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Leonard Maboko, alipokuwa akizungumza na wanahabari baada ya uwasilishwaji wa maeneo maalum ya uwekezaji kuhusu mapambano dhidi ya Ukimwi ili kuweza kupata matokeo chanya katika afua (mikakati) ya kupambana na kudhibiti maambukizi hayo.

Alisema tume hiyo inafanya mapitio ya nakala maalum inayopambanua maeneo ya kipaumbele ambayo nchi inahitaji kuwekeza zaidi katika kupambana na Ukimwi ili kufikia lengo la dunia la kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

"Katika tathmini iliyofanyika imeonekana ni programu nzuri ambayo itasaidia kufikia malengo ya kidunia ifikapo 2030 yanayohamasisha kusiwe na maambukizi mapya, kondomu zikiwafikia walengwa na watu wakitumia vizuri basi tutafikia azma hiyo," alisema Dk. Maboko.

Mkurugenzi huyo alisema suala la tohara kwa wanaume na kudhibiti biashara ya ngono kwa wanawake kama yatafanyiwa kazi ipasavyo itaweza kupunguza maambukizi hayo.

Akizungumzia kuhusu tiba, Dk. Maboko alisema eneo hilo linaonekana kuleta matumaini makubwa kwa ajili ya kupunguza vifo kwa kuwa moja ya lengo ifikapo mwaka 2030 ni kuhakikisha vifo vinavyotokana na Ukimwi vinafikia sifuri.

"Hili suala la kupunguza vifo linaenda sambamba na namna watu wanavyotumia dawa kwa zaidi ya asilimia 50 tukapunguza maambukizi mapya lakini pia tukapunguza vifo vinavyotokana na Ukimwi," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alisema wizara itahakikisha kuwa huduma za kinga zinayafikia makundi yote kwa kuwa ni jukumu la serikali na wadau wengine wa maendeleo kutoa huduma bora za kinga kwa wakati.

Dk.Subi alibainisha kuwa ni muhimu kwa kila mtu kuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kupima na kujua hali ya afya na kuchukua tahadhari za kutowaambukiza wengine.

Aidha, alisema licha ya maambukizo ya Ukimwi kupungua mapambano zaidi yanahitajika.

Alisema nakala hiyo imeandaliwa na Tacaids na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi(UNAIDS) na itapitiwa na wadau mbalimbali kutoka serikalini na washirika wa maendeleo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (kushoto), akimwapisha aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma, Edward Mpogolo kuwa Mkuu mpya wa Wilaya ya Ikungi, mkoani humo jana, baada ya kuteuliwa na Rais Dk. John Magufuli kushika nafasi hiyo, iliyoachwa wazi na Miraji Mtaturu aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Vijana wazalendo wampongeza JPM

Na Renatha Msungu, DODOMA

UMOJA wa vijana wazalendo wa vyuo vikuu mkoani Dodoma wamempongeza Rais John Magufuli, kwa jitihada za kuleta maendeleo nchini na kuwataka Watanzania kuwapuuza wanaobeza kazi zake. Pongezi hizo zilitolewa jana na mwenyekiti wa umoja huo, Jerry Motella, alipokuwa akizungumza baada ya maandamano ya kumpongeza Rais Magufuli kupokelewa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma.

Motella alisema serikali ya awamu ya tano imefanya mambo mengi mazuri, ambapo hawana budi kuunga mkono na kwamba kama vijana wana imani na serikali hiyo.

"Ndio maana tumeamua kutoa tamko hili ili kupongeza yale yote uliyowafanyia vijana wa taifa hili na tunawaomba Watanzania kuwapuuza wale wote wanaotaka kukwamisha juhudi za kuleta maendeleo ya taifa hili," alisema.

Alisema Rais amefanya mambo makubwa kwenye sekta nyingi nchini huku kwa upande wa vyuo vikuu serikali imeongeza wigo wa udahili wa wanafunzi jambo ambalo limetoa fursa kubwa ya wanafunzi kujiunga na elimu ya juu. Akizungumza baada ya kupokea maandamano hayo, Mkuu wa Wilaya Patrobas Katambi, alisema kuna watu wanabeza jitihada za Rais, lakini wanamsifu kwa hatua yake ya kukutana na marais wa nchi jirani Chato na kurejesha fedha na dhahabu zilizokuwa zimetoroshwa kupitia Kenya.

Aliwapongeza vijana kwa hatua hiyo na kuwataka kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano na kuwataka kuwashughulikia wale wote wanaombeza Rais mitandaoni.

"Wanaongoza kubeza kulalamika na kunong'ona dhidi ya serikali hii wanapochunguzwa inabainika wamesimama misingi mikuu mitatu ambayo ni uchu wa kumiliki mali, nafasi na nguvu kinyume na misingi ya serikali inayoongozwa na Dk. Magufuli," alisema.

Katambi alimwomba Rais aendelee kuchukua hatua ya kuwatumbua usiku na mchana pia na yeye kama ataonekana hatoshi kwenye nafasi hiyo ilimradi wapatikane viongozi wanaofaa kwa maslahi ya taifa.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd (katikati), akikabidhi mashuka ya kulalia wagonjwa kwa Waziri wa Afya, Hamad Rashid (wa pili kulia), kwa ajili ya hospitali za vitongoji, yaliyotolewa na mfanyabiashara Said Nassir Bopar (kushoto), wilayani Wete, Pemba juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Zanzibar yang'ara kimataifa utalii

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

SEKTA ya utalii visiwani Zanzibar imeendelea kudhihirisha ubora wa huduma zinazotolewa na hoteli mbalimbali kutokana na kushinda tuzo zaidi za kimataifa.

Safari hii, hoteli ya Dream of Zanzibar iliyoko Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, imeng'ara katika shindano la 26 linalotoa tuzo za hoteli bora kwa huduma za kitalii duniani upande wa Afrika na nchi zilizo katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

Dream of Zanzibar inakuwa hoteli ya nne kutoka Zanzibar kutwaa tuzo za ubora, baada ya Mnemba, Melia na Essque Zalu zilizoshinda tuzo za kimataifa kwa vipindi tafauti na kuwa miongoni mwa hoteli 10 bora nchini Tanzania.

Akizungumza katika hafla ya kusherehekea tuzo hiyo iliyofanyika juzi hotelini hapo, Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, aliupongeza uongozi na wafanyakazi wa Dream of Zanzibar kwa ushindi huo, akisema unaisogeza Zanzibar katika kituo kikuu cha utalii ililojiwekea.

Waziri Kombo alisema ni ukweli usiopingika kwamba Zanzibar inayo fursa ya kushindana kama kituo kikuu cha utalii duniani.

"Ninaamini sana kuwa hii si ndoto ya mchana na kwa ushirikiano uliopo baina ya sekta ya umma na binafsi, tutapaa kileleni na kufika mbali tukitembea juu ya mawingu," alisema.

Alisema Zanzibar imebarikiwa vivutio mbalimbali zikiwamo rasilimali za baharini ambazo zinaruhusu ubunifu wa bidhaa zenye ubora zinazoweza kuingia kwenye ushindani utakaoimarisha mikakati inayolenga kupokea watalii wenye hadhi kubwa na watumiaji wa kiwango cha juu.

Kombo alisema kuna umuhimu kwa Wazanzibari kuitambua na kuithamini historia nzuri na ya kipekee ya nchi yao na kusisitiza kwamba wasipoizungumza wenyewe, hakuna mtu mwingine kutoka nje atakayefanya kazi hiyo.

Aidha, aliwataka kujivunia tuzo zinazopatikana kupitia sekta ya utalii, ambazo alisema pia zinaitangaza Zanzibar miongoni mwa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, Afrika na ulimwengu kwa jumla. Aliwahakikishia wawekezaji wa sekta ya utalii kuwa milango ya wizara yake iko wazi kwao kujadili na kubadilishana mawazo juu ya namna bora ya kuimarisha utalii.

Pia alisema serikali chini ya Rais Dk. Ali Mohamed Shein imejizatiti kufikia utalii wa daraja la juu.

Naye Meneja Mkuu wa hoteli hiyo yenye hadhi ya nyota nne, Reda Sweed, alisema tuzo waliyopata ni matokeo ya kujitolea, uvumilivu na ushirikiano wa wafanyakazi na viongozi wote wa kampuni hiyo.

Alisema anaamini kuwa tuzo hiyo itasaidia kuitangaza zaidi Zanzibar kuwa ni kituo kikuu na bora kwa watalii kutembelea.

"Pamoja na furaha tuliyonayo kwa ushindi wetu, hatutabweteka bali huu ni mwanzo wa kubuni mbinu mpya za kuimarisha hoteli yetu kufikia hatua nyengine kubwa zaidi, ambayo itawavutia wageni wengi kuliko sasa," alisema Sweed.

Aliahidi kuwa ifikapo Julai, mwakani, wataibua mikakati mipya na mizuri zaidi itakayoiongezea hadhi hoteli yao na kuendelea kuleta tuzo zingine kadiri itakavyowezekana.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Sabaha Saleh Ali, watendaji wengine na wadau wa sekta ya utalii kutoka hoteli na kampuni mbalimbali nchini.

SMZ yageukiwa kilimo cha kahawa

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema itaendelea kuwahamasisha wakulima hususan vijana kujikita katika kilimo cha kahawa ambacho kinaendana na mahitaji ya soko la dunia.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano kuhusu maonyesho ya matumizi (unywaji) wa kahawa yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 30-31 mjini Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali khamis Juma, alisema kahawa imekuwa na matumizi makubwa hususan kwa wageni, hivyo itakapozalishwa kwa wingi itawanufaisha wakulima.

Pia alisema vijana watakapojikita katika kilimo hicho, watajikwamua na ukosefu wa ajira ambao unarejesha nyuma malengo yao ya maendeleo.

Juma alisema amechukua fursa hiyo kutoa wito kwa wawekezaji kuwekeza katika kilimo hicho ili kuimarisha upatikaji wa zao hilo pamoja na kuongeza ukuwaji wa matumizi ya mazao ya asili ndani ya nchi.

Hata hivyo, aliitaka Bodi ya Kahawa Tanzania kuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi na taasisi mbalimbali juu ya umuhimu wa utumiaji wa zao hilo ili kuimarisha afya zao.

Kuhusu Siku ya Maonyesho ya Unywaji wa Kahawa na mashindano ya kutafuta kahawa safi, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa Tanzania, Ameir Hamza, alisema lengo la kuwapo siku hiyo ni kuwahamasisha wananchi kutumia kahawa ili kuimarisha afya zao.

Alisema pia maonyesho ni njia mojawapo ya kutangaza mazao ya asili yaliyopo Tanzania na kutangaza utamaduni wa namna ya kuandaa kahawa ya Tanzania visiwani inayowavutia wageni wa nchi mbalimbali.

Ameir alisema maonesho hayo yatashirikisha wageni wa nchi za Afrika ili kuimarisha ushirikiano walio nayo na kutangaza ubora wa kahawa iliyoko Tanzania.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa African Fine Coffee Association (AFCA), Samuel Kamau, alisema wanaendelea na jitihada mbalimbali za kutafuta soko la uhakika la zao hilo ili kuwanufaisha wakulima.

Alisema taasisi yao itaendelea kuwaelimisha wakulima ili kuzalisha kahawa yenye ubora ambayo itauzwa katika nchi mbalimbali na kutumika kwa wengi nchini.

Zaidi ya watu 400 kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Afrika Kusini, wanatarajiwa kushiriki katika maonyesho hayo yanatarajiwa kufanyika katika kiwanja cha hoteli ya Sea Cliff.

Awaonya watendaji kujitwalia misaada

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewatahadharisha watendaji wa taasisi za umma wanaopata misaada na vifaa kutoka kwa wahisani kuacha tabia ya udokozi wa vifaa hivyo inayoweza kupunguza nguvu za kuungwa mkono kwao.

Alisema vifaa na misaada hiyo lazima isimamiwe katika kutoa huduma za muda mrefu na kwamba kinyume chake ni kuwavunja moyo wahisani na wafadhili wanaoamua kujitolea kusaidia taasisi hizo.

Balozi Iddi alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na viongozi na watendaji wa hospitali za vitongoji na Abdullah Mzee katika hafla ndogo ya kutoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya hospitali hizo na sekta ya kilimo vilivyotolewa na mfanyabiashara maarufu Said Bopar.

Alisema iko mifano hai iliyowahi kutokea kwa baadhi ya watendaji wakiwamo pia viongozi wa sekta ya afya kujichukulia misaada na vifaa vilivyotolewa na wafadhili pamoja na wahisani, jambo ambalo alisema ni udhaifu unaokera na kuchukiwa na jamii.

Makamu huyo alimshukuru na kumpongeza Bopar kwa uzalendo wake wa kusaidia zaidi sekta za elimu kilimo na afya maeneo muhimu yanayotoa huduma kubwa zaidi kwa wananchi wengi hasa vijijini.

Alisema wako wafanyabiashara wenye uwezo mkubwa zaidi ya Bopar ambao wana wajibu na stahiki ya kuunga mkono jitihada kama hizo ili jamii iondokane na changamoto zinazoikabili ambazo zimo ndani ya jamii yenyewe.

Kuhusu stahiki za wafanyakazi wa afya hasa katika baadhi ya Hospitali ya Wilaya za Pemba, Makamu wa Pili wa Rais alikemea tabia ya baadhi ya viongozi kuchelewesha posho za watendaji wao wanaowajibika hata katika muda wa ziada.

Elimu afya ya uzazi yatakiwa kuanzia msingi

Elizabeth Faustine, MWANZA

ELIMU ya afya ya uzazi inatakiwa kufundishwa kuanzia ngazi ya shule za msingi, ili watoto wakike waweze kujitambua na kuondokana na changamoto ya mimba za utotoni. Hayo yalielezwa na Meneja Miradi wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Nicodemus Eatlawe, wakati akizungumza na Nipashe, na kusema mabadiliko yaanzie kwenye sera ya elimu.

Eatlawe alisema mitaala pamoja na sera ya elimu nchini inapaswa kubadilishwa ili kuondokana na changamoto ya mimba za mapema kwa kuongeza suala la afya ya uzazi kufundishwa kuanzia elimu ya msingi.

“Suala la kupungua kwa mimba za utotoni ni ndoto kwa sababu sio la mtu mmoja bali zinahitajika jitihada za pamoja kati ya serikali na wadau wengine, hivyo inahitaji sera zaidi ambayo ukiizungumzia unaingia ndani kabisa katika mitaala,” alisema Eatlawe.

Alisema mbali na elimu hiyo kufundishwa shuleni, pia wazazi wanapaswa kuwafundisha na kuwaelimisha watoto wao kuhusu mabadiliko ya mwili na afya ya uzazi. “Watoto wengi hawajui mabadiliko ya mwili na namna mimba inavyopatikana, hivyo mitaala itakapobadilika na kuongeza suala la elimu ya afya ya uzazi kuanza kufundishwa kuanzia ngazi ya elimu ya msingi kwa kuwa itasaidia kutatua changamoto hiyo,” alisema Eatlawe. Alisema katika jitihada za kuhakikisha changamoto hiyo inapungua, mtandao huo unapendekeza na kushauri yafanyike mabadiliko katika sera ya taifa ya elimu na mitaala ili elimu ya uzazi ifundishwe kuanzia shule za msingi, na kwamba yapo mashirika mengine ambayo yamekwenda shuleni na kuanzisha jumuiya za watoto wa kike.

Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika Mei 31 mkoani hapa, Ofisa Elimu Mkoa wa Mwanza, Michael Ligola, alisema, kwa kipindi cha mwaka 2018, jumla ya wanafunzi wa kike 402 walikatisha masomo kutokana na ujauzito.

“Kati ya hao waliokatisha masomo yao kutokana na ujauzito, wanafunzi 103 walitoka shule za msingi huku sekondari wakiwa 309 kutoka halmashauri nane za Mkoa wa Mwanza,” alisema Ligola.

Mambo muhimu Tanzania kupata watalii zaidi China

Na Beatrice Philemon

UJUMBE wa wafanyabiashara kutoka Jimbo la Zhejiang, China uliokuja nchini umesema Tanzania itafanikikwa kupata watalii wengi zaidi kutoka kwenye jimbo ikiwa na miundombinu mizuri.

Miundombinu hiyo inahusisha magari ya kutosha kubeba watalii, hoteli za kutosha na ndege ya moja kwa moja kutoka Tanzania hadi Zhejiang.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Thomas Mihayo wakati wa mkutano wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji kati ya wafanyabiashara kutoka Zhejiang na wafanyabiashara wa Tanzania.

“Tumefurahi sana kupata ujio wa wafanyabiashara kutoka Zhejiang ambao tumekutana nao leo na wametuahidi kutangaza vivutio vyetu vya utalii katika Jimbo la Zhejiang ili kusaidia Tanzania kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kujionea vivutio vya utalii wetu,” alisema.

Alisema ili Tanzania iweze kupata watalii wengi zaidi kutoka majimbo ya China, tayari kampuni ya wakala wa utalii ya ‘Touchroad International Holdings Group kutoka Jimbo la Shanghai, China limesaini Mkataba wa Makubaliano na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kuleta watalii kutoka China. “Kuanzia Agosti, kila wiki kampuni hii itakuwa inaleta watalii kutoka China kwa kutumia ndege ya kukodi ya ATCL kwa sababu bado hakuna ndege ya moja kwa moja ya kuleta watalii kutoka China na sasa ATCL ipo kwenye mchakato wa kuanzisha ruti za kwenda China,” alisema. “Kupitia makubaliano hayo, tunatarajia idadi ya watalii kutoka Zhejiang na majimbo mengine ya China itaongezeka na pia Tanzania kujulikana zaidi kwa vivutio vya utalii,” alisema.

Alisema haya ni matokeo ya ziara iliyofanyika Novemba mwaka 2018 na TTB kwa kushirikiana na wadau wengine waliopo katika sekta ya utalii waliokwenda katika majimbo ya Hong Kong, Beijing, Shanghai, Guangzhou na Shanghai kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania na kutangaza safari za ndege mpya za ATCL zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni katika ya Tanzania na China.

Alisema lengo kuu la ziara hii ya utangazaji utalii ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaongeza sehemu ya umiliki wa soko kwenye soko la utalii la China kwa kutangaza vivutio vya utalii, fursa za uwekezaji zilizopo nchini na safari mpya za ndege za ATCL kwenda China.

Pia aliomba Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kuangalia jinsi wafanyabiashara wa Tanzania wanavyoweza kuwekeza China kwa sababu wafanyabiashara kutoka DongYoung wameomba Watanzania kwenda kuwekeza katika eneo hilo.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Vodacom Tanzania Plc, Nandi Mwiyombella, akionyesha simu mpya aina ya Tecno Yente iliyozinduliwa kwa ushirikiano kati ya Vodacom na Tecno jijini Dar es Salaam, jana. **MPIGAPICHA WETU**

Wateja Vodacom wawezeshwa kuingia ulimwengu wa kijiditali

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya mawasiliano ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania, imeungana na kampuni ya Tecno kuwawezesha wateja wake kwa kuwaletea toleo jipya la simu aina mbili za Tecno Yente na Itel Bamba.

Uzinduzi huu ni harakati ya Vodacom kuhakikisha jitihada zake za kuwezesha maisha ya kidijitali kwa wateja wao, kwa kupitia simu janja zinafanikiwa.

Akizungumza na waandishi wakati wa uzinduzi wa simu hizo jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa matukio wa kampuni ya Tecno, Anuj Khosla, alisema:

“Tumedhamiria kuhakikisha kila Mtanzania anamiliki simu janja na kwa pamoja tunalifanya taifa la Tanzania kuwa la kidijitali.”

“Simu hizi zitapatikana kwa bei ya Sh. 75,000 kwa Itel Bamba - 3G na Shilingi 195,000 kwa TECNO Yente ambayo ni - 4G, simu zote mbili zinakuja na ofa, ambapo kwa simu ya Itel Bamba wateja wetu watapata GB 3 kila mwezi kwa miezi minne na kwa simu ya TECNO Yente watapata GB 2 kila mwezi kwa mwaka mzima,” alisema.

“Tunafuraha kushirikiana na TECNO kuendelea kuimarisha zaidi azimio letu la kuzidi kuwawezesha wateja wetu kuwa katika ulimwengu wa kidijitali. Uzinduzi huu umekuja katika kipindi mwafaka, hasa kwa kuwa Watanzania wengi zaidi wanatumia huduma za simu janja,” alisema Nandi Mwiyombella, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Vodacom Tanzania.

Mwiyombella alisema zaidi kuwa: “Katika zama hizi za kidijitali, kupata taarifa, kununua na kulipia vitu, na kupata burudani za muziki na sinema, vinawezekana kwa kutumia simu janja, na matoleo haya mapya ya TECNO Yente na ITEL Bamba yatawezesha hayo yote na zaidi.

Uzinduzi huu umekuja sambamba na msimu wa sikukuu ya Nanenane ili kuhakikisha wateja wetu, ambao ndiyo kipaumbele chetu wanasherehekea sikukuu ya Nanenane msimu huu kidijitali zaidi.”

Alisema simu hizo zitapatikana katika maduka yote ya Vodacom Tanzania na pia katika madawati ya huduma kwa mteja yanayotoa huduma kwa wateja wa kampuni hiyo maeneo mbalimbali nchini.

HABARI KIMATAIFA

Johnson aanza kazi akutana na Baraza la Mawaziri

LONDON, Uingereza

WAZIRI Mkuu mpya wa Uingereza, Boris Johnson jana, alikutana na baraza lake jipya la mawaziri, wakati ambapo anakabiliwa na kazi ngumu ya kuileta nchi yake pamoja iliyogawika kwa kiwango kikubwa.

Johnson aliahidi kuuondoa mkwamo wa Brexit uliosababisha kujiuzulu kwa Waziri Mkuu wa hapo awali, Theresa May.

Muda mfupi baadaye baada ya kukutana na Baraza la Mawaziri alitoa taarifa bungeni kuhusu mipango yake ya kuiondoa Uingereza kutoka Umoja wa Ulaya (EU).

Waziri Mkuu huyo mpya aliliambia baraza lake jipya la mawaziri kwamba Uingereza imo katika kipindi nyeti kabisa cha historia ya nchi hiyo. Johnson kwa mara nyingine alisisitiza azma ya kuiondoa Uingereza kutoka EU itakapofika Oktoba, 31 au hata kabla ya hapo.

Hata hivyo, Waziri Mkuu huyo anatarajiwa kukabiliwa na maswali magumu atakapolihutubia bunge.

Mwanasiasa huyo amebakiwa na siku100 ili kuweza kuitimiza ahadi ya kuutekeleza mchakato wa Brexit, baada ya kusema kuwa serikali ya waziri mkuu wa hapo awali ilipoteza muda wa miaka mitatu kutokana na kutojiamini katika suala la Brexit. Kwa upande wake kiongozi wa Ireland, Leo Varadkar alisema kwamba Johnson ataweza kufanya mazungumzo na EU juu ya kufikia mkataba mpya wa Brexit.

Naye kiongozi wa Chama cha Democratic Unionist Party (DUP), Arlene Forster, alisema matokeo ya kura ya maoni juu ya Brexit yanapaswa kutekelezwa.

Wakati huo huo, kiongozi wa chama cha Labour, Jeremy Corbyn alimtaka Johson akubali kuitisha uchaguzi utakaompa uhalali wa kuongoza nchi.

Lakini Johnson alisema kuwa haoni ulazima wa kuitisha uchaguzi kabla ya kutekeleza mchakato wa kuiondoa Uingereza EU.

Katika baraza jipya la mawaziri Johnson aliwateua watu aliowahi kufanya nao kazi ikiwa pamoja na Waziri mpya wa Mambo ya Nje, Domic Raab, Waziri wa Fedha, Sajid Javid, Waziri wa Mambo ya Ndani, Priti Patel na Mnadhimu wa chama cha Kihafidhina bungeni, Jacob Rees-Mog. **DW**

Rais wa Marekani, Donald Trump (kulia), akiwa pamoja na mwanamfalme wa Saud Arabia wakishika chati inayoonyesha mauzo ya silaha. **PICHA: REUTERS**

Trump akaidi amri ya Bunge, auza silaha Saudia

RIYADHI, Saudi Arabia

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametumia kura ya turufu kufutilia mbali uamuzi wa Bunge la Congress la kuzuia mauzo ya silaha yenye thamani ya Dola bilioni nane kwa Saudia na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Rais Trump alisema kuwa maamuzi hayo matatu yatadhoofisha uwezo wa Marekani ulimwenguni na kuharibu uhusiano wake na washirika wake.

Hatua hiyo inajiri baada ya mabunge yote mawili kupiga kura ya kuzuia mauzo hayo.

Baadhi ya wabunge walieleza kuwa walihofia silaha hizo huenda zikatumiwa dhidi ya raia katika mgogoro wa Yemen.

Wabunge hao pia wameshutumu vitendo vya Saudia nchini Yemen pamoja na mauaji ya mwaka jana ya mwandishi, Jamal Khashoggi.

Hata hivyo, Bunge la Seneti litapiga kura baada ya muda wa siku moja ili kuona iwapo litakaidi uamuzi wa Rais Trump, kulingana na kiongozi wa wengi katika chama cha Republican, Mitch Connel.

Lakini wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kuwa kuna uwezekano mkubwa Bunge la Seneti halitakuwa na theluthi tatu ya kupinga uamuzi huo wa Rais Trump.

Hii ni mara ya tatu kwa Rais Trump kutumia uwezo wake tangu alipochukua mamlaka.

Mei mwaka huu Ikulu ya Marekani ilitangaza hali ya dharura ya kitaifa kukaidi uamuzi wa wabunge hao na kupitisha mauzo hayo ya silaha.

Wakati huo, Rais Trump alieleza kuwa alifanya uamuzi huo kutokana na vitisho vinavyotolewa na Iran.

Lakini hatua hiyo ilizua upinzani mkali kutoka kwa wale waliohofia kwamba silaha hizo zitatumiwa dhidi ya raia nchini Yemen na vikosi vya Saudia.

Wabunge wakiwamo wa Republican katika Bunge la Seneti pia walisema kwamba kulikuwa hakuna sababu muhimu ya kukaidi maamuzi ya Congress.

Hata hivyo, Rais Trump akitumia kura yake ya turufu na kupendekeza kuwa kuzuia uuzaji wa silaha hizo kutaendeleza mgogoro wa Yemen kwa muda mrefu na kwamba raia wengi wataathirika nchini humo.Pia alisisitiza kuwa Saudia na UAE zinapinga vitendo vya Iran na washirika wake katika eneo hilo.

Hali ya wasiwasi kati ya Marekani na Iran imeongezeka tangu Rais Trump ajiondoe katika makubaliano ya nyuklia ya Iran ili kuzuia mpango wa Iran.

Marekani imeeleza kuwa iliangusha ndege isio na rubani ya Iran wiki iliopita na imelaumu Iran kwa msururu wa mashambulizi dhidi ya meli za mafuta katika Ghuba.

Nayo Iran iliangusha ndege isio na rubani ya Marekani mwezi Juni. **BBC**

Chanjo ya ebola yazua kizaazaa

KINSHASA, Congo

SIKU chache baada ya kujiuzulu kwa Waziri wa Afya nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) akidai ni kutokana na kuingiliwa majukumu yake, baadhi ya wanasiasa wameeleza wasiwasi wao kuhusu kutumika kwa chanjo ya ebola ambayo haijafanyiwa majaribio.

Mkanganyiko huo umetokea wakati watu zaidi ya 1,700 wakiripotiwa kupoteza maisha kutokana na virusi vya ugonjwa wa ebola. Mbunge mmoja wa mashariki mwa nchi hiyo, Muhindo Nzangi Butondo, aliibuka na kuwataka wananchi wake kutokubali kupewa chanjo hiyo ambayo haijathibitishwa.

Butondo akinukuliwa na vyombo vya habari vya kimataifa, alisema hataki kuona wananchi wake wanatibiwa kama nguruwe wa Guinea, akitaka chanjo mpya iliyoanza kutolewa ithibitishwe.

Butondo alionya dhidi ya kutengenezwa kwa mfumo mwingine wa afya nchi humo ambao hautawajengea uwezo maofisa wa afya wa ndani, matamshi anayoyatoa baada ya waziri wa afya aliyejiuzulu Dk. Olly Ilunga kudai kusikitishwa na serikali kukubali kuanza kutumika kwa chanjo mpya ambayo haikupitia mifumo sahihi ya kiafya. **RFI**

Waziri Masauni ashtushwa uhaba wa mbwa JNIA

Na Romana Mallya

UPUNGUFU wa mbwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), umemshtua Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ambaye amemwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro kuhakikisha idadi yao inaongezwa kwenye viwanja vyote nchini.

Akiwa kiwanjani hapo jana katika ziara ya kikazi, Masauni alielezwa kuwa idadi ya mbwa wenye mafunzo maalum ya kunusa na kubaini vitu ni wanne wakati uhitaji uliopo ni mbwa 16.

Masauni alifanya ziara hiyo uwanjani hapo ikiwa ni siku moja baada ya Rais John Magufuli kushuhudia makabidhiano ya kilo 35.267 za dhahabu zilizokamatwa Februari 15, mwaka jana katika Uwanja wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta, Nairobi nchini Kenya.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, Masauni alisema kitendo cha kukamatwa kwa dhahabu hiyo kimetia aibu vyombo vya dola hususani Jeshi la Polisi na vile vinavyoshughulika na usalama.

"Nimekuja hapa kuangalia hali ya usalama wiwanja vya ndege hii ni baada ya Rais Magufuli jana (juzi) kupokea dhahabu kutoka Kenya. Nimeona upungufu baada ya ziara yangu moja wa askari wa mbwa wenye mafunzo na sifa, ninamuagiza IGP kwa haraka ahakikishe anaongeza idadi ya askari mbwa wenye sifa ili kuongeza ufanisi wa viwanja vyetu. Hili lifanyike kwenye viwanja vyote vya ndege nchini," alisema.

Pia alisema idadi ya mbwa inatakiwa iongezwe hasa serikali inapokaribia kuhamia kwenye jengo jipya la tatu la kimataifa uwanjani hapo ambalo litakuwa na idadi kubwa ya abiria na changamoto nyingi.

"Rais Magufuli ameajiri askari wapya hivi karibuni, lazima katika kitengo cha askari mbwa nacho kifanye kazi zake, kwa kutilia mkazo suala hili, viwanja vyote vya ndege vihakikishe vinakuwa na askari mbwa wa kutosha wenye sifa vinginevyo hatutakuwa na sababu ya kuwa na watu kwenye kitengo hiki. Nitakifumulia mbali tuweke watu wengine," alisema.

Masauni alisema serikali imedhamiria kuokoa rasilimali za nchi kwa kuhakikisha kila mtu kwenye nafasi yake anatekeleza majukumu yake.

Pia Masauni alimtaka IGP Sirro ahakikishe kuna kuwa na ushiriki wa askari wa vyombo mbalimbali kwenye ukaguzi wa mizigo na abiria kwenye viwanja vya ndege.

"Tumekubaliana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kufanya marekebisho ili kuwepo kwa ushiriki wa askari wetu kwenye ukaguzi wa mizigo na abiria, tumekubaliana mfumo wa ushiriki wao uboreshwe," alisema na kuongeza:

"IGP Sirro ahakikishe watu wanaoletwa hapa wawe wa kutosha na wawe na vigezo na sifa za kuweza kubaini vitu vinavyopitishwa uwanja wa ndege na vinavyotarajia kupitishwa na wahalifu yakiwamo madini, dawa za kulevya na nyara za serikali."

Awali, Inspekta Omar Lunyombe kutoka kikosi cha mbwa uwanjani hapo, alisema mbwa waliopo uwanjani hapo ni wanne ambao wanakagua dawa za kulevya zikiwamo Cocaine, Heroine pamoja na pembe za ndovu.

Kamanda wa Polisi Viwanja vya Ndege Tanzania, ACP Jeremiah Shila, alisema IGP Sirro aliahidi kununua mbwa wengine na mchakato umeshaanza ndani na nje ya nchi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhi cheti kwa Mkuu wa Kitengo cha Kibenki cha Taasisi za Sekta ya Umma, Noelina Kivaria ikiwa ni utambuzi wa mchango wa benki hiyo, katika kufanikisha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jumuiya za Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), uliofanyika jijini Mwanza hivi karibuni. Kushoto ni Mwenyekiti wa Alat Taifa, Gulamhafeez Mukadam. Benki hiyo ilikuwa ni moja ya wadhamini wa mkutano huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

Benki ya NBC yaahidi ushirikiano zaidi Alat

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NBC imeahidi kuendelea kutoa huduma bora zenye ubunifu kwa Mamlaka za Serikali ya Mtaa (Alat), ili kuongeza tija na ufanisi zaidi kwa mamlaka hizo.

Ahadi hiyo ilitolewa na Meneja Mahusiano ya Kiserikali wa NBC, William Kallaghe, wakati akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa 35 wa Mwaka wa ALAT jijini Mwanza hivi karibuni.

Alisema katika kipindi cha miaka 50 ya uwapo wa benki hiyo nchini, imewekeza katika huduma mbalimbali za kifedha ambazo zimeleta tija kubwa kwa mamlaka hizo na taifa kwa ujumla.

"Katika kipindi chote hicho NBC tumefanikiwa kutoa suluhisho ya kiubunifu kupitia huduma za kielektroniki kwa Halmashauri za Wilaya na Manispaa katika ukusanyaji wa mapato sambamba na huduma za malipo zinazoboresha usahihi katika uendeshaji akaunti," alisema.

Alibainisha kuwa uwezo huo umeimarishwa zaidi kufuata mfumo wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG), Mtandao wa NBC Wakala, Mfumo wa makusanyo wa POS pamoja na makusanyo kupitia simu za mikononi.

Kwa mujibu wa Kallaghe, huduma za kielektroniki za malipo na ukusanyaji wa mapato zinazotolewa na benki ya NBC kwa mamlaka hizo zimeongeza ufanisi katika malipo na ukusanyaji wa mapato kwa mamlaka hizo, hivyo kurahisisha usahihi katika uendeshaji wa akaunti zao.

"Matawi ya NBC yamewezeshwa kwa nyanja zote katika kufanikisha mahitaji yote ya kifedha kwa Halmashauri na Mamlaka zote za serikali ya mitaa," alibainisha huku akiongeza kuwa lengo kuu ni kuhakikisha mamlaka hizo zinatoa huduma bora na za kisasa sambamba na kujiongezea mapato.

'Tujibebe' kuelimisha vijana ujasiriamali

Na Mwandishi Wetu

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Vodacom Tanzania Foundation imeungana na Taasisi ya Kimataifa ya Girl Effect kuzindua 'Tujibebe' huduma mpya inayotoa elimu ya maisha kupitia simu ikiwalenga vijana waliopevuka wenye umri kati ya 15-19.

Huduma ya Tujibebe itawaunganisha vijana wenye uzoefu katika ujasiriamali kuwahamasisha wengine na kusaidiana kutatua changamoto za maisha wakati wakitimiza malengo yao.

Maudhui ya Tujibebe yanalenga kuwapa vijana wa Kitanzania taarifa na rasilimali wanazohitaji kufanya maamuzi sahihi ya maisha yao, mafunzo ya kuboresha ujuzi wao, kuanzisha biashara na kusimamia fedha zao.

Tujibebe itatumia tovuti pamoja na huduma za simu za IVR kutoa mafunzo kupitia simulizi ya sauti ambayo ni bure kupitia mtandao wa Vodacom.

Jukwaa la Tujibebe limezinduliwa rasmi na Mjumbe wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Simon Shayo na wadau mbalimbali wa sekta ya maendeleo.

Shayo alisema amefurahi kuona kampuni nyingi zimeungana ili kuhakikisha usawa wa kijinsia unaongezeka na pia kuwawezesha vijana kiuchumi.

Alisema serikali inafanya kazi na taasisi mbalimbali ikiwamo UNDP, USAID na Vodacom Tanzania Foundation katika masuala ya kuleta usawa na kuwawezesha wasichana.

"Sote tunafahamu kwamba teknolojia ya simu ina uwezo wa kubadilisha dunia, tunafuraha sana kuungana na Girl Effect, kupitia mtandao wetu ambapo tutaweza kuwafikia vijana wengi zaidi na kuwafanya wafikie malengo yao," alisema Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia.

Akielezea faida za jukwaa la Tujibebe katika kuleta mabadiliko katika maisha ya vijana wa kitanzania, Mkurugenzi Mtendaji wa Girl Effect, Jessica Posner Odede, alisema maudhui ya tujibebe yametengenezwa kwa ajili ya kuwaunganisha vijana wote, lakini lengo kubwa ni kubadilisha maisha ya wasichana watakaotumia elimu kutoka Tujibebe. "Mara nyingi vijana huwa na maswali mengi kuhusiana na kesho yao, na hawajui mahali pakupata majibu sahihi."

MATANGAZO MCHANGANYIKO

ELIMU/ MASOMO

NAFASI ZA MASOMO, Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO KAWE
(S.M.M. 1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya Mwanzo: **MJINI TANGA**
Usimamizi wa Mirathi No**. 69/2019**

Ombi la **HAMISI MALIKI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **RUKIA BIWTHAMISI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **12/7/2019.**

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **12/07/2019.**

115342102

KUPOTEA KWA VYETI



115341002

Meshack Muganyizi anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0841/0199** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Humura, cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.0109-0776** kilichotolewa Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Ihungo na cheti cha kuzaliwa chenye namba **C/No02164903.** Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **UDSM/RB/5308/2017**

KUPOTEA KWA CHETI



115341202

Misanga Abdala Hassan anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1619/0113** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Victory, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **UD/RB/1563/2019**

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TANGAZO

FORM II

Katika Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini

USIMAMIZI WA MIRATHI NO 79……2019,

Ombi la Kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi
Usimamizi wa miradhi ya Marehemu
DR. Fulgence Mosha.

Kwa: Yeyote anaehusika

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhuthuria kesi wakitaka mnao tarehe 16-08-2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 23-07-2019

115341502

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
wilaya ya DODOMA
MADAI NAMBARI 171/2019
MDAI WILLIAM JACKSON CHANZENZE
MDAIWA KUSAJA NZINDO
Kwa KUSAJA NZINDO
KIJIJI CHA MAKANDA/ TINAI

Kwa kuwa mdai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TSH. 24,500,000/=

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 13/08/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25/07/2019

115341602

KUPOTELEWA NA KADI YA GARI.

Jafari Sitta Nyanda anatangaza kupotelewa na Kadi ya gari aina ya Toyota Kluger yenye namba za usajili T 139 DKZ yenye Engine No. **2AZ1603122** na Chassis No. **ACU200111165.**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa katika Kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi
KAH/RB/ 581/2019.

115341102

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

EVERTON YAJITOSA KUMWANIA ZAHA

LONDON, England

KLABU ya Everton imeingia kwenye mbio za kumwania mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, baada ya mchezaji huyo kuweka wazi kwamba anataka kuondoka pale Goodison Park.

Everton imeingia kwenye mbio hizo huku Arsenal nayo ikiwa inamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa udi na uvumba. Kwa mujibu wa Sky Sport, Everton inajiandaa kutuma ofa ya pauni milioni 55 kwa Crystal Palace kwa ajili ya kumsajili winga huyo.

Huku Arsenal ikisuasua kuhusu bajeti ya usajili wa mchezaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto, Everton sasa inataka kuwapiku na kumsajili nyota huyo.

Chanzo kimoja kilichopo karibu na mchezaji huyo, kimedokeza kwamba, Zaha mwenyewe anataka kuondoka klabuni hapo.

Arsenal kwa mara ya kwanza walitoa ofa ya pauni milioni 40 kwa ajili ya kumsajili Zaha, lakini ilikataliwa.

Idrissa Gueye sasa kutua PSG

PARIS, Ufaransa

KLABU ya Everton imefikia makubaliano ya kulipwa pauni milioni 28 ili kumuuza kiungo wake, Idrissa Gueye kwenda Paris Saint Germain.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal kwa muda mrefu alikuwa akiwania na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa na sasa wameamua kumchukua mazima.

Hata hivyo, usajili wa mchezaji huyo unaweza kuchelewa, kutokana na mambo kadhaa ambayo yanatakiwa kukamilishwa kwanza kabla ya kufikia makubaliano ya kumsajili.

Aidha, imeripotiwa kuwa tayari Gueye na PSG wameshafikia makubaliano ya maslahi binafsi kwa ajili ya kutua jijini Paris.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye amekuwa na kiwango cha kuvutia aliwasili klabuni hapo mwaka 2016, na sasa inaaminika kwamba anataka kwenda kupata changamoto mpya katika klabu nyingine.

Na pia ameripotiwa kuwa ana shauku kubwa ya kutaka kucheza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Gueye aliweka wazi mpango wa kutaka kuondoka hapo Goodison Park kwenda PSG Januari mwaka huu.

Mchezaji huyo wa zamani wa Aston Villa amebainisha wazi mpango wake wa kutaka kwenda kucheza Paris.

Hata hivyo, ujio wa Fabian Delph hapo Everton kutoka Manchester City unaonekana ndio sababu kubwa kwa Gueye kutaka kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto.

Ayew akamilisha usajili

LONDON, England

KLABU ya Crystal Palace imekamilisha usajili wa kudumu kwa mshambuliaji, Jordan Ayew baada ya kucheza kwa mkopo kutoka Swansea.

Ayew mwenye umri wa miaka 27, msimu uliopita aliwachezea kwa mkopo Eagles hao na sasa atarudi katika dimba Selhurst Park baada ya kukubali kusaini mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo.

Ayew alifunga bao moja katika mechi 20 za Ligi Kuu na sasa ataichezea tena klabu hiyo msimu huu.

"Kwa hakika nina furaha kubwa, nilifurahia msimu uliopita," alisema Ayew akinukuliwa na cpfc.co.uk.

"Nilifurahia mandhari ya uwanja, mashabiki na wachezaji wenzangu, kila kitu kilikuwa sawa kabisa kwa upande wangu na nimeamua kuendelea kuitumikia Crystal Palace."

Kocha wa Palace, Roy Hodgson ambeinisha kuridhishwa kwake na kiwango cha Ayew na kusema kwamba atakuwa na mchango mkubwa kwa timu hiyo.

"Tuna furaha kubwa kukamilisha usajili wa Jordan tutakuwa nae tena hapa kwa misimu mitatu na ataendelea kucheza hapa Crystal Palace," alisema.

"Alijiimarisha yeye mwenyewe na kuonyesha kiwango cha juu na aliisaidia timu kwa kipindi chote alichocheza na sisi hapoa."

HABARI MICHEZO

Klopp amkataa Coutinho Liverpool

LIVERPOOL, England

JURGEN Klopp ametupilia mbali uwezekano wa Philippe Coutinho kurudi kwenye dimba la Anfield, akisisitiza kwamba mshambuliaji huyo anatakiwa kujiimarisha yeye mwenyewe pale Barcelona.

Coutinho tangu atue Camp Nou miezi 18 iliyopita kiwango chake kimeonesha kushuka licha ya kubeba mataji mawili ya Ligi Kuu na miamba hao wa Katalunya.

Barcelona imekuwa ikijaribu kutaka kumuuza Coutinho kwenda Paris Saint-Germain huku wao wakitaka kumrudisha Neymar na hivi karibuni alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Liverpool.

Lakini Klopp ameiambia ESPN kwamba hakuna uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kurudi klabuni hapo badala yake anatakiwa kujiimarisha kwenye Ligi hiyo ya Hispania.

"Kiukweli Phil Coutinho anaweza kuisaidia timu yoyote duniani, kwani bado yupo fiti kwa asilimia 100," amesema Klopp.

"Sio kuhusu hilo. Nampenda Phil, nafikiri ni mchezaji mzuri, lakini kumsajili tena itatakiwa kutumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha.

"Na hilo haliwezekani. Kwa sasa ni bora zaidi akaendelea kucheza Barcelona na kuweza kujiimartisha kwa kiwango chake."

USAJILI WA GRIEZMANN UNAWEZA KUZUIWA

MADRID, Hispania

USAJILI wa mchezaji Antoine Griezmann kutoka Atletico Madrid kwenda Barcelona unaweza kuzuiwa kutokana na mzozo wa malipo, kwa mujibu wa BBC Sport.

Uwezekano wa kutokea hatua hiyo umedokezwa na rais wa ligi kuu ya Hispania, La Liga, Javier Tebas.

Atletico Madrid imetuma malalamiko baada ya Barcelona kutangaza kumsajili Griezmann kwa kukubali kutoa kitita cha euro milioni 120 kama matakwa ya mkataba wa mchezaji huyo ulivyoainisha Julai 12 mwaka huu. Bei ya mchezaji huyo kimkataba ilishuka kutoka yuro milioni 200 hadi milioni 120 Julai Mosi mwaka huu.

Hata hivyo, Atletico wanaamini kuwa Barcelona na Griezmann walikubaliana kuhusu usajili mapema mwaka huu na kusubiri ifike Julai Mosi ili bei yake ipungue.

"Inawezeka kuzuia uhamisho wa mchezaji," Tebas ameuambia mtandao wa Onda Cero. "La Liga itabidi iamue nini cha kufanyika katika sakata hili."

Griezmann tayari ameshacheza mchezo mmoja wa kirafiki na klabu yake mpya ya Barcelona, ambapo walifungwa 2-1 na Chelsea nchini Japan.

Tebas amesema: "Atletico wamewasilisha malalamiko yao na wameonesha namna gani kuna mashaka ya kuwapatia Barcelona leseni ya Griezmann.

"Tayari kuna mchakato wa kulitatua hili, na wale ambao wanalisimamia itabidi waeleze namna ya utatuzi wake."

Atletico iliiripoti Barcelona kwa chombo kinachosimamia soka duniani, Fifa, kwa madai ya kumfuata kinyume cha sheria Griezmann Disemba mwaka 2017.

Mchezaji huyo alikataa kujiunga na Barcelona mwaka mmoja uliopita.

Milinkovic-Savic akaribia kutua Manchester United

LONDON, England

SERGEJ Milinkovic-Savic anakaribia kujiunga na Manchester United baada ya wakala wake ambaye pia ni mchezaji wa zamani wa Chelsea, Mateja Kezman kuripotiwa kusafiri kwenda jijini London kwa ajili ya mazungumzo.

Kiungo huyo kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England na ameripotiwa kwamba ndiye mbadala wa Paul Pogba kama akiondoka hapo Old Trafford.

Na sasa wakala wa Milinkovic-Savic, Kezman, ambaye aliichezea Chelsea mechi 41 ametua nchini England kwa ajili ya kukamilisha uhamisho wake kutoka klabu ya Lazio kwa mujibu wa gazeti la Gazzetta dello Sport.

Taarifa zaidi zinasema kuwa klabu zote mbili, Lazio na Man United zimekubaliana ada ya uhamisho ya pauni milioni 71 kwa ajili ya mchezaji huyo ili azibe pengo la Pogba.

Pobga raia wa Ufaransa amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Old Trafford, huku timu za Real Madrid na Juventus zikitajwa kumuwania.

Milinkovic-Savic, ambaye alifunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho 41 akiichezea Lazio msimu uliopita, alikuwa anawaniwa na United tangu msimu uliopita wakati Jose Mourinho akiwa kocha pale.

Mwaka jana Milinkovic-Savic aliongeza mkataba wake na Lazio ambao utamfanya akae hapo hadi mwaka 2023 na mapema mwezi huu, rais wa klabu hiyo, Claudio Lotito alisema kwamba itakuwa vigumu kwake kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA

TOTTENHAM VITANI KUMWANIA DYBALA

Yajiandaa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kukamilisha usajili wa straika huyo...

TURIN, Italia

KLABU ya Tottenham imeanza mawasiliano na Juventus kwa ajili ya kumsajili straika Paulo Dybala, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 80.

Usajili huu wa kushtukiza ambao unaonekana kuwekewa nguvu zaidi na timu hiyo iliyopoteza mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mabosi wa klabu hiyo wameeleza wako tayari kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kumnasa mshambuliaji huyo.

Ofisa mmoja wa Spurs ambaye yuko jijini Turin kwa ajili ya kuzungumza na Juventus kuhusiana na uhamisho wa straika huyo mwenye umri wa miaka 25, amesema wako tayari kuvunja rekodi ya usajili ya klabu yao ambayo waliiweka mapema katika kipindi cha majira ya joto mwaka huu, ili kufanikisha nyota huyo anatua London Kaskazini.

Dybala, ambaye pia ni mchezani wa Timu ya Taifa ya Argentina, anatajwa kuwa ni mmoja kati ya washambuliaji bora duniani kwa sasa na endapo atafanikiwa kutua Spurs, Mauricio Pochettino atakuwa ameimarisha kwa kiwango kikubwa kikosi chake.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo ameonekana kuwa katika wakati mgumu tangu Cristiano Ronaldo alipotua Juventus, msimu uliopita alifanikiwa kufunga mabao 10, na klabu hiyo ya Italia inafikiria kujiandaa kupokea ofa mbalimbali kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji huyo.

Huku wakiwa wamefanikiwa kumsajili, Tanguy Ndombele kutoka Lyon mapema mwezi huu, Spurs pia imejikita katika kuhakikisha inafanikiwa kumnasa Dybala katika klabu yake na inatarajia kutenegeneza "pacha" pamoja na mshambuliaji mwingine wa timu hiyo, Harry Kane.

Imefahamika kuwa, mawasiliano kuhusu usajili wa nyota huyo yalianza tangu mwezi uliopita, kupitia kwa mwenyekiti wa timu hiyo, Daniel Levy ambaye amehitaji kumwongezea nguvu kocha wa timu hiyo, ingawa Manchester United na Paris Saint-Germain zote zimetajwa kuwa kwenye mbio za kumwania straika huyo.

Februari mwaka jana kabla Spurs haijacheza na Juventus katika mechi ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Pochettino alisema kuwa : 'Kila siku ni vizuri kucheza dhidi ya timu nzuri duniani," kocha huyo alisema maneno hayo kabla ya kutambua kipaji cha Dybala kuwa ni cha kipekee.

ZISIKUPITE

GUEYE AKARIBIA PSG

MABOSI wa Paris St-Germain wamekubali kulipa kiasi cha pauni milioni 28 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Senegal na Everton, Idrissa Gueye, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Mail)***

ZAHA ATAKIWA EVERTON

EVERTON ambayo ni maarufu kwa jina la The Toffees inatarajia kukamilisha mazungumzo na Crystal Palace ili kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye thamani ya pauni milioni 80. ***(Sky Sports)***

KLOPP AMKATAA COUTINHO

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ameahirisha uamuzi wa kumrejesha katika kikosi chake kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho (27), ambaye aliondoka Anfield mwaka 2018 kwa dau la pauni milioni 142. ***(ESPN)***

BRUCE: LONGSTAFF HAONDOKI

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce, ameiambia Manchester United kuwa hawana nafasi ya kumsajili kiungo raia wa England, Sean Longstaff, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Star)***

BAILLY NJIA PANDA

BEKI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Eric Bailly (25), anahofia kuwa mhanga wa mchakato wa usajili wa beki wa kati wa Leicester na England, Harry Maguire, ambaye anatarajia kujiunga na klabu hiyo ya Old Trafford. ***(Metro)***

PEPE KUMRITHI LUKAKU

MANCHESTER United imemtaja mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Nicolas Pepe (24), ambaye thamani yake ni pauni milioni 70, kuwa ndiye mrithi wa straika wa Ubelgiji, Romelu Lukaku ambaye anakaribia kujiunga na Inter Milan. ***(Times)***

LUKAKU AWEKWA PEMBENI

STRAIKA Romelu Lukaku (26), amekubali kuwekwa pembeni katika mechi za maandalizi ya msimu mpya zinazochezwa na Manchester United ili kutoharibu mchakato wake wa usajili wa kuelekea Inter Milan ambao utahusisha dau la pauni milioni 75. ***(Sun)***

KHEDIRA ANUKIA WOLVES

MABOSI wa Wolves wameanza mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Juventus , Sami Khedira (32). ***(Sky Sports Italia via Football Italia)***

SERGEJ AANZA KUAGA

KIUNGO wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic (24), ameweleza wachezaji wenzake kuwa ataondoka klabuni hapo katika majira ya joto huku kukiwa na tetesi za kutakiwa na Manchester United. ***(Il Tempo via Express)***

WOLFSBURG, LEIPZIG VITANI

KLABU za Wolfsburg na RB Leipzig zimeonyesha nia ya kumsajili kwa mkopo, winga wa Arsenal, Emile Smith Rowe, ambaye ana umri wa miaka 18. ***(Independent)***

KOSCIELNY MATATANI

BEKI Mfaransa Laurent Koscielny (33), atalazimishwa kufanya mazoezi na timu ya vijana ya Arsenal licha ya kikosi cha kwanza cha timu hiyo tayari kimesharejea England baada ya kumaliza ziara ya Marekani. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

ZFF, KLABU PEMBA SASA KIMEELEWEKA

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), vilabu vya Ligi Kuu visiwani hapa na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba vimefikia makubaliano na sasa vilabu hivyo vimeahidi vitashiriki katika ligi mbalimbali zinazoandaliwa na shirikisho hilo, imeelezwa.

Kikao cha makubaliano kati ya pande hizo mbili kilifanyika jana kwenye Ukumbi wa Gombani ambacho kilimalizika kwa mafanikio ya soka ya Zanzibar.

Ilielezwa kuwa klabu hizo za Pemba zilitaka kuhakikishiwa madai yao kufanyiwa kazi, jambo ambalo limetatuliwa na ZFF.

Katika barua yao ya Julai 6 mwaka huu, klabu hizo zilisema kuwa zinahitaji kupatiwa kanuni, kufahamu kama ligi ina mdhamini na klabu zitapata nini kutoka kwa wadhamini hao na vile vile walikuwa gharama za uhamisho wa wachezaji kutoka nje ya Zanzibar, ambazo ni Sh. milioni 1.5 kwa sasa zipungue.

Madai mengine ya klabu hizo kutounga mkono uamuzi wa kushusha daraja kwa timu sita kati ya klabu 16 zinazoshiriki Ligi Kuu na kueleza kwamba kanuni hiyo itaziumiza zaidi timu zinazotoka Pemba kutokana na kutokuwa na fedha za kupambana ikilinganishwa na wenzao wa Unguja.

Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, ambaye amechaguliwa kukiongoza chama hicho mapema mwezi uliopita, alilazimika kuitisha kikao ili kumaliza sintofahamu hiyo.

Pandu alisema kuwa kupitia makubaliano hayo, tayari klabu zote zimethibitisha kwa maandishi kwamba zitaanza taratibu za maandalizi ya msimu mpya. Alisema pia viongozi hao wameridhika na maelezo waliyopatiwa katika kikao hicho ambacho Pandu aliambatana na Katibu Mkuu wa ZFF, Mohammed Hilal "Tedy" na kukubali kushiriki ligi za msimu ujao.

Khamis Hamad Khamis, kiongozi wa Mwenge FC, alisema kuwa wamefurahi kufikia muafaka kutoka kwa rais huyo wa ZFF, jambo ambalo walifikiria awali lisingewezekana.

"Hapo awali tulifikiria kama tunaonewa, ndio maana tukatoa malalamiko yetu kwa barua na tukataka majibu pia yarudi kwa barua, ila kutokana na mweleko tuliofahamishwa, mambo yamekwenda vizuri na sasa tunaamini tumepata kiongozi bora katika soka letu," alisema Khamisi.

Naye Katibu Mtendaji wa FFC, Ramadhan Dadi, alisema kuwa wanashukuru sana kukutana na rais na wanatarajia kupata mazuri kutoka kwake katika kuendesha soka la Zanzibar na kumuomba atekeleze ahadi ambazo alizitoa wakati anaingia madarakani.

Zahera kurejea nchini kesho

Na Faustine Feliciane

WAKATI kambi ya Yanga ikiendelea kupamba moto mkoani Morogoro, Kocha Mkuu wa timu hiyo Mkongomani Mwinyi Zahera, anatarajiwa kuwasili nchini kesho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema kuwa licha ya kutokuwapo nchini, kocha huyo alikuwa akitoa maelekezo ambayo yalikuwa yanafanyiwa kazi katika programu za mazoezi.

"Kocha anarejea nchini Jumamosi na siku inayofuata (Jumapili) ataondoka Dar es Salaam na kuja huku (Morogoro) kambini ili kuendelea na majukumu yake," alisema Saleh.

Mratibu huyo aliongeza kuwa timu ikiwa chini ya Kocha Msaidizi, Noel Mwandila, inaendelea na programu zake za mazoezi na wamebakisha michezo miwili ya kirafiki kabla ya kikosi kurejea Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki katika tamasha lao la Siku ya Wananchi.

Katika hatua nyingine, akizungumzia suala la wachezaji waliogoma kujiunga na kambi, Saleh, alisema kuwa suala la wachezaji hao linafanyiwa kazi na uongozi wa timu hiyo.

Wachezaji ambao wapo nje ya kambi ya timu hiyo bila taarifa na ruhusa ya klabu ni pamoja na Kelvin Yondani, Juma Abdul na Andrew Vincent 'Dante'.

Katika tamasha lake ambalo litafanyika kwa mara ya kwanza, Yanga itacheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Kariobang Shark kutoka Kenya.

Black Sailor FC yasonga mbele

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Black Sailor imefanikiwa kusonga mbele katika bonanza la Ujamaa baada ya kuifunga Kundemba mabao 3-0 kwenye mechi ya ufunguzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Mabao ya Black Sailor katika mechi hiyo iliyokuwa na ushindani wakati wote, yalipachikwa na Nurdin Mohammed, Saleh Mshamu na Fauzi Abdallah.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa Black Sailor, Mshamu, alisema matarajio yao ni kuona wanachukua ubingwa wa bonanza hilo na vile vile kutumia michezo hiyo kujiandaa na msimu mpya.

Mshamu alisema kuwa siri ya wao kupata matokeo mazuri ni wachezaji kujituma na kuiona mechi hiyo sawa na fainali.

"Tumeanza vizuri, wachezaji tulijituma lakini malengo yetu ni kuchukua kombe hili, japo timu zinazoshiriki zote ni nzuri na zimejipanga vema," alisema Mshamu.

Bonanza hilo la Ujamaa ambalo ni la tatu kufanyika mwaka huu, limeandaliwa na Klabu ya Ujamaa na linashirikisha timu 16 ambazo zinacheza kwa mtindo wa mtoano.

Mkurugenzi wa Uendeshaji SportPesa, Luca Neghesti akikabidhi mbegu za nyasi mpya kwa Wizara ya Michezo kuchangia maboresho ya sehemu ya kuchezea ya Uwanja wa Taifa. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Yusuf Singo. **NA MPIGAPICHA WETU**

Azam FC, Eagle Noris uwanjani

Na Shufaa Lyimo

KATIKA kuendelea kujiimarisha kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa, Azam FC, wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Eagle Noris kutoka Burundi itakayochezwa leo kwenye uwanja wa Azam Complex.

Azam ambayo imerejea nchini wiki iliyopita ikitokea Rwanda katika mashindano ya Kombe la Kagame, imepangwa kuanza na Ethiopia 1 ya Ethiopia, kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa timu hiyo, Jafferi Idd, alisema kuwa wanaamini mechi hiyo ya leo itaendelea kuwaweka wachezaji wao tayari kukabiliana na ushindani kwenye msimu mpya unaotarajiwa kuanza mapema mwezi ujao.

Iddi alisema kuwa benchi la ufundi la timu hiyo linafurahi kuona kila mchezaji anajituma katika mazoezi, ili kujihakikishia namba katika kikosi cha kwanza.

"Timu inaendelea vizuri na mazoezi yake, na kesho (leo) Ijumaa tutakuwa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Eagle, ni katika mwendelezo wa maandalizi yetu ya msimu mpya," alisema Jaffer.

Kiongozi huyo alisema pia, hali za wachezaji wote wa timu hiyo zipo vizuri na kudai kila mmoja ana morali ya kufanya vizuri katika msimu mpya wa Ligi Kuu Bara ambao utaanza ifikapo Agosti 23 mwaka huu.

Micheze
Ijumaa Julai 26, 2019
Nipashe

Everton yajitosa kumwania Zaha UKURASA 28

Raheem Sterling wa Manchester City akimpiga chenga golikipa wa Kitchee, JQ Guo, wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo juzi, nchini China. Man City iliibuka na ushindi wa mabao 6-1. **PICHA: MTANDAO**

Kilomoni akamatwa, aachiwa na polisi

●●● Alikuwa akifanya mkutano na waandishi bila kibali, atakiwa kuandika barua...

Na Shufaa Lyimo

MWANACHAMA wa Simba, Hamisi Kilomoni, jana, alikamatwa na Jeshi la Polisi kabla ya kuachiwa huru kwa kosa la kufanya mkutano na waandishi wa habari bila kibali.

Kilomoni alikamatwa nyumbani kwake Kinondoni Block 41 na kupelekwa katika kituo cha polisi cha Oysterbay ambako alishikiliwa kwa muda.

Hata hivyo, baadaye Kilomoni aliachwa huru na kurejea nyumbani kwake na kuwaeleza waandishi wa habari kwamba, ametakiwa kuomba kibali cha kufanya mkutano huo.

Awali kabla ya kuanza kuzungumza alisitishwa na kuamuriwa na polisi kuelekea kituo cha Polisi Oysterbay Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Waandishi walimwomba azungumze kidogo kabla ya kupanda kwenye gari la polisi alisema, ameshangazwa na kitendo cha polisi kuja nyumbani kwake na kudai haijawahi kutokea.

"Mimi nashangaa kuona polisi wamekuja kwangu wananichukua wanasema sina kibali cha kuzungumza na waandishi wa habari," alisema Kilomoni kabla ya kupanda gari la polisi.

Alisema kila mara anapotaka kuzungumza na waandishi wa habari huwa anafanyia kwake, kutokana na yeye hali yake kiafya sio nzuri.

"Mimi huwa nafanyia mkutano hapa hapa kwa sababu mimi ni mgonjwa kwa muda mrefu," alisema.

Ndairagije: Kenya sio wa kuwabeza

Na Faustine Feliciane

LICHA ya kufanya maandalizi mazuri kuelekea kwenye mchezo wa kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) dhidi Kenya (Harambee Stars), Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars'), Etienne Ndayiragije, amesema kuwa wapinzani wao si wa kuwabeza.

Taifa Stars inatarajia kuikaribisha Harambee Stars keshokutwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na zitarudiana baada ya wiki mbili nchini Kenya. Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije, alisema kuwa anafurahishwa na hamasa ya kila mchezaji kwenye timu hiyo na kueleza kwamba wataingia uwanjani wakiwa tofauti na wanavyofahamika.

Ndayiragije alisema kuwa lengo la kubadilisha mfumo wa uchezaji, ni kutaka kuwachanganya Harambee Stars ambayo wanafahamiana baada ya kukutana katika mashindano mbalimbali.

"Tutachukua tahadhari kubwa katika mechi hiyo, Kenya nao watakuja kamili kupambana ili kuweza kupata matokeo mazuri, ipo mbinu ambayo naendelea kuwapa wachezaji wangu kuelekea katika mchezo huo ambao ni muhimu," alisema Ndayiragije.

Aliongeza kuwa anafahamu wapinzani wao wapo vizuri na wanacheza kwa kutumia nguvu zaidi, lakini hana wasiwasi kwa sababu amejiandaa kwa kila mbinu kuhakikisha hawafanyi makosa katika mchezo huo muhimu.

"Kikubwa wachezaji wameonyesha hali ya kutamani ushindi, wanafuata kile ambacho nawaelekeza mazoezini, kwa siku zilizobakia ni kuwaweka sawa, stamina yao ni nzuri na kwa kifupi, wako tayari kwa mchezo huo," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002